

Ksh 3800/=

**MABADILIKO YA MAUDHUI KIWAKATI KATIKA
NYIMBO ZA HARUSI ZA JAMII YA WAEMBU**

NA

NJERU S. MBOGO

**Tasnifu hii imetolewa ili kutosheleza baadhi ya mahitaji ya shahada ya
uzamili katika Chuo Kikuu cha Kenyatta.**

2008

Mbogo, Njeru S.
*Mabadiliko ya maudhui
kiwakati katika*



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

UNGAMO


Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kutolewa kwa mahitaji ya shahada katika Chuo Kikuu kingine chochote.



27/10/08


NJERU S. MBOGO

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi wa Chuo Kikuu cha Kenyatta.



27/10/2008

PROF. GEOFFREY K. KING'EI



DKT. CHATHERINE M. NDUNGO

YALIYOMO

Ukurasa

Yaliyomo.....	i
Tabaruku.....	iv
Shukrani	v
Iksiri	vi
Maana ya istilahi muhimu.....	viii

SURA YA KWANZA

1.0 Utangulizi.....	1
1.0.1 Usuli wa mada ya utafiti	1
1.0.2 Chimbuko la Waembu	2
1.0.3 Eneo la jamii ya Waembu kijiografia	3
1.0.4 Jamii ya Waembu kabla ya maingilio ya wakoloni	4
1.2 Swala la utafiti.....	5
1.3 Maswali ya utafiti.....	6
1.4 Nadharia tete	7
1.5 Malengo ya utafiti	7
1.6 Sababu za kuchagua mada	8
1.7 Upeo wa utafiti.....	10
1.8 Misingi ya nadharia.....	10
1.8.1 Nadharia ya uhalisia.....	11

1.8.2 Nadharia ya ufeministi	16
1.8.3 Nadharia ya ufeministi wa Kiafrika.....	17
1.9 Yaliyoandikwa kuhusu mada	21
1.10 Mbinu za utafiti	30
1.11 Sampuli	32
1.12 Mbinu za kukusanya data.....	33
1.13 Mbinu za uchanganuzi wa data.....	33
1.14 Uwasilishaji wa matokeo	34
1.15 Hitimisho.....	34

SURA YA PILI

2.0 Utangulizi.....	35
2.1 Maudhui ya nyimbo za harusi.....	35
2.2 Maudhui katika nyimbo za baada ya harusi.....	43
2.3 Hitimisho.....	56

SURA YA TATU

3.0 Utangulizi.....	57
3.1 Nyimbo za baada ya maingilio ya wakoloni na maudhui yake	58
3.2 Hitimisho.....	77

SURA YA NNE

4.0 Utangulizi.....	78
4.1 Maudhui ya kabla ya maingilio ya wakoloni.....	78
4.2 Maudhui ya baada ya maingilio ya wakoloni	80
4.3 Mabadiliko ya maudhui	82
4.4 Hitimisho.....	89

SURA YA TANO

5.0 Utangulizi.....	90
5.1 Muhutajari wa tasnifu.....	90
5.2 Hitimisho.....	91
5.3 Mapendekezo	92
Marejeleo.....	95
Kiambatisho I.....	99
Kiambatisho II.....	102
Kiambatisho III	103
Kiambatisho IV	104
Kiambatisho V	105

TABARUKU

Naitabarukia tasnifu hii kwa Bibi yangu Valerian Gicuku kwa kunipa ari na motisha wa kuyaendeleza masomo yangu hadi kiwango hiki.

SHUKRANI

Namshukuru Mola kwa kunijalia na kunipa siha nzuri iliyoniwezesha kuendelea na masomo yangu ya uzamili hadi mwisho.

Pili, nawatolea shukrani za dhati wasimamizi wangu katika kazi hii Prof. Geoffrey K. King'ei na Dkt. Catherine M. Ndungo kwa kuniongoza, kunishauri na kunihimiza niendelee na kazi hii.

Tatu ningependa kuwashukuru wahadhiri wote katika idara ya Kiswahili na Lugha nyinginezo za Kiafrika, Chuo Kikuu cha Kenyatta, haswa walioniongoza hadi lengo langu likatimia.

Shukrani zangu za dhati ziwaendee kwa wale wote waliochangia utafiti huu kwa kuniimbia nyimbo zilizonipa data ya utafiti.

Mpiga chapa wa kazi hii Bwana Muriuki pia namshukuru sana.

Mwisho nawashukuru wasomi wenzangu Kyamba, Mogaka, Kanini, Wathome na Rajwai kwa kunipa mwelekeo ulipohitajika pamoja na kunipa moyo kuendelea na kazi hii.

IKSIRI

Malengo ya utafiti huu yalikuwa kuonyesha jinsi maudhui katika nyimbo za harusi miongoni mwa watu wa jamii ya Waembu yalivyobadilika kiwakati tangu kabla na baada ya maingilio ya Wakoloni. Aidha, utafiti huu umechunguza na kueleza matukio ya kijamii yaliyochangia mabadiliko haya. Bali na hayo, utafiti huu umelenga kueleza mabadiliko haya ya maudhui kinadharia.

Kwa kuzingatia nadharia ya uhalisia iliyoasisiwa kwa pamoja na Gustav Flaubert (1850), Rene Wellek na wengine kati ya karne ya 19 na 20, ilibainika kwamba maudhui katika nyimbo kama utanzu wa fasihi simulizi hubadilika kusadifu matukio ya kihistoria ya kipindi fulani katika jamii.

Kipindi cha kabla ya maingilio ya wakoloni katika jamii ya Waembu kilikuwa na nyimbo anuwai za harusi zilizobeba maudhui mahususi. Baada ya maingilio ya wakoloni, maudhui katika nyimbo hizi yalibadilika kwa kiasi kikubwa ingawa kuna machache yaliyoendelea.

Kwa sababu ya mabadiliko hayo, kumezuka mitazamo miwili ya kuangalia maudhui katika nyimbo za harusi za jamii ya Waembu ambayo ni maudhui ya nyimbo za kabla ya maingilio ya wakoloni na ya zile za

baada ya maingilio hayo. Utafiti huu umeonyesha jinsi maudhui katika nyimbo za harusi za jamii ya Waembu yalivyobadilika kutoka kipindi kimoja hadi kingine.

MAANA YA ISTILAHU MUHIMU

Maingilio ya wakoloni: katika utafiti huu, neno hili lilitumiwa kumaanisha athari za jumla zilizopatikana katika jamii ya Waembu ambazo zilichangia kuanguka kwa utamaduni wa Waembu na kuanza kutekeleza shughuli zao “kimagharibi”.

Kabla ya maingilio ya wakoloni: utafiti huu unatumia istilahi hii kumaanisha kipindi ambacho utamaduni wa jamii ya Waembu ulikuwa imara bila athari za kimagharibi zilizochangiwa na wakoloni.

Wakoloni: katika utafiti huu neno hili litatumia kumaanisha wazungu waliosababisha utamaduni wa Waembu kupata athari za kimagharibi ikiwa ni dini pamoja kuacha tamaduni zao kwa kiasi kikubwa na kufuata tamaduni za wazungu.

Uhalisia: Utafiti huu ulitumia istilahi hii kumaanisha nadharia ya uhakiki wa fasihi inayochambua fasihi kwa kuihushisha na uhalisia (ukweli) unaopatikana katika maisha ya jamii.

Ufeministi wa Kiafrika: Utafiti huu ulitumia istilahi hii kumaanisha nadharia inayo mwangazia mwanamke katika mwelekeo wa Kiafrika: jinsi jamii kwa jumla inavyomtazama mwanamke.

USULI WA MADA YA UTAFITI

Utafiti wa mada wa jamii za Kiafrika nyimbo za kuanzishaji wa kwanza koteleza majukumu kadhaa bila pingazaji. Finnegan (1970) alitazunguza mada hii ayimape kwa shughuli nyingi za binadamu kama: kuzikwa, kupatilia, kurika, tohara, baraka, uvuvi h.k., mshirikishi wa utafiti. Nyimbo hizi huwa na maudhui na ulindo ya kipekee wa jamii za shughuli zozoteleza. Finnegan (1970) alitazunguza mada hii na ndiye katika nyimbo hizi hutadilika na wakati ambapo wakati wa wakati wake na mwelekeo wa jamii kwa jumla.

SURA YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI

Sura hii imeshughulikia maswala ya kimsingi yanaofaa kuzingatiwa wakati wa kuandika tasnifu. Baadhi ya mambo haya ni pamoja na usuli wa mada ya utafiti, asili ya jamii ya Waembu, eneo la jami ya Waembu kijiografia, jamii ya Waembu kabla na baada ya maingilio ya wakoloni, swala la utafiti, maswali ya utafiti, nadharia tete, malengo ya utafiti, sababu za kuchagua mada hii, upeo wa utafiti, misingi ya nadharia, yaliyoandikwa kuhusu mada ya utafiti, mbinu za utafiti na sampuli. Sura hii imehitimishwa kwa kujadili mbinu za uchanganuzi wa data.

1.0.1 USULI WA MADA YA UTAFITI

Katika muundo wa maisha wa jamii za Kiafrika nyimbo za kitamaduni zilitumiwa kutekeleza majukumu kadhaa bila pingamizi. Finnegan (1970) aunga mkono kauli hii asemapo kuwa shughuli nyingi za binadamu kama vile, kulima, kupalilia, kuzika, tohara, harusi, uvuvi n.k., hushirikisha nyimbo na uimbaji. Nyimbo hizi huwa na maudhui na mitindo ya kipekee inayohusiana na shughuli inayotekelezwa. Finnegan (1970) asema kuwa maudhui na mitindo katika nyimbo hizi hubadilika na wakati ambapo husawiri historia ya wakati wake na mwelekeo wa jamii kwa jumla.

Nandwa na Bukenya (1983) waeleza sababu za mabadiliko ya maudhui na mitindo ya nyimbo katika jamii za Kiafrika wasemapo kuwa kazi yoyote ya fasihi haitokei katika ombwe tupu, bali huchota maudhui katika jamii. Mabadiliko ya hali ya maisha katika jamii huenda sambamba na mabadiliko ya maudhui katika kazi ya fasihi, haswa fasihi simulizi. Utanzu wa nyimbo ni baadhi ya tanzu zilizokumbwa na mabadiliko kama haya.

Mchango wa Nandwa na Bukenya (1983) ni muhimu kwa utafiti huu, kwani unatuangazia sababu zinazochangia kuwepo na mabadiliko ya maudhui katika nyimbo za harusi za jamii ya Waembu yaliyotokea kiwakati (kihistoria).

1.0.2 CHIMBUKO LA WAEMBU

Asili ya Waembu, ikiwa ni pamoja na jamii zingine za Kibantu wanazopakana nazo, huhusishwa na baadhi ya wanahistoria na misitu ya Kongo (Were na Wilson 1991). Kulingana na nadharia ya Kongo, inadaiwa kuwa Waembu, Wakikuyu, Wameru, Wapokomo, Mijikenda, Wakamba na jamii zingine zinazohusiana, zilihama kutoka Kongo na kuingia nchini Kenya kupitia katikati ya ziwa Victoria na milima ya Taita. Baadaye jamii hizo zilihamia pwani ya Kenya na kukusanyika mahali palipoitwa Shungwaya kati ya karne ya kumi na mbili na kumi na tano (Spear 1978). Baada ya kuishi Shungwaya kwa muda wa miaka

kadha wa kadha, mkusanyiko huu wa watu ulivunjika kufuatia ongezeko la idadi ya watu ambalo lilisababisha ukosefu wa chakula. Aidha palizuka ugonjwa ambao uliwafanya watu kutorokea sehemu mbali mbali.

Jamii ya Waembu ilihama kuelekea wilaya ya Embu wanapoishi hadi hii leo.

1.0.3 ENEO LA JAMII YA WAEMBU KIJIOGRAFIA

Wilaya ya Embu ni mojawapo ya wilaya kumi na tatu za mkoa wa Mashariki. Eneo la wilaya ya Embu ni kilomita 729.49 mraba. Wilaya hii inapakana na wilaya ya Mbeere kwa upande wa mashariki na kusini mashariki, wilaya ya Kirinyaga upande wa magharibi na wilaya ya Tharaka kwa upande wa kaskazini. Wilaya ya Embu ina Tarafa tano ambazo ni Manyatta, Runyenjes, Kyeni, Nembure na "Central" (Tarafa ya kati). Tarafa hizi zina lokesheni kumi na tano na kata hamsini na mbili.

Watu wa jamii ya Waembu ndio wakaazi asili wa wilaya ya Embu. Wilaya ya Embu huwa katika eneo lenye mvua ya kutosha ya kati ya milimita 1,495 na 1,700 kwa mwaka. Hali ya joto huwa kati ya 12°C Julai na 27.1°C Machi. Mchanga katika wilaya ya Embu huwa na rutuba ya kutosha jambo, linaloweza kilimo cha aina mbalimbali kama cha

kahawa, majani ya chai, pamoja na pareto kushamiri. Watu wengi wa jamii ya Waembu huishi mashambani wakitekeleza shughuli za kilimo.

Wilaya ya Embu huwa na milima na mabonde mengi ambayo kwa kiasi yanazuia mawasiliano. Mito minne muhimu katika wilaya ya Embu ni Thuchi, Kii, Ruringazi na Ena.

1.0.4 JAMII YA WAEMBU KABLA NA BAADA YA MAINGILIO YA WAKOLONI

Watu wa jamii ya Waembu, kama ilivyo jamii yoyote ya Kiafrika, walitekeleza shughuli zao kitamaduni kabla ya wakoloni kuingia (Ngugi 1983). Nyimbo zilizoimbwa katika shughuli mbalimbali za kijamii zilikuwa za kitamaduni. Nyimbo hizo zilikuwa na maudhui yaliyoshabihiana na uhalisi wa maisha ya jamii ya wakati huo.

Nyimbo hizi zilibeba maudhui maalum yaliyoziwezesha kutekeleza majukumu yake ya wakati huo ambayo yalikuwa na mwelekeo wa kitamaduni (Ngugi 1983).

Baada ya maingilio ya wakoloni dini, haswa ya Kikristo, ilisambaa miongoni mwa watu wa jamii za Kiafrika. Utamaduni wa jamii hizi ulianza kupata athari za kimagharibi, asasi za kitamaduni pamoja na vikorombwezo vya kitamaduni viliporomoka (P'Bitek 1986). Mambo

haya yalibadilisha mwelekeo wa maisha ya watu wa jamii za Kiafrika, ya Waembu ikiwemo. Athari za kimagharibi zilipatikana katika mambo mengi ya kijamii yaliyotekelezwa kitamaduni hapo awali.

Mielekeo ya watu kuhusu shughuli mbalimbali zilizotekelezwa kitamaduni ilianza kubadilika, haswa baada ya watu kukengeuka na kuonekana kama tamaduni zilizopitwa na wakati.

Kabira na Karega (1988) wasema kuwa nyimbo kama utanzu wa fasihi simulizi hubadilika kiwakati. Kwa hivyo ni muhimu kutalii jinsi mabadiliko haya yanavyotokea na sababu za mabadiliko hayo.

1.2 SWALA LA UTAFITI

Utafiti huu umeshughulikia mabadiliko ya maudhui kiwakati katika nyimbo za harusi miongoni mwa jamii ya Waembu. Mabadiliko haya yameangaliwa katika misingi ya mitazamo miwili kimaudhui ambayo ilitawala nyakati mbalimbali katika jamii ya Waembu. Mitazamo hiyo ni maudhui ya kabla ya maingilio ya wakoloni na baada ya maingilio ya wakoloni.

Tafiti mifano zimefanywa ambazo kwa kiasi kikubwa zimelingana na utafiti huu, hata hivyo tafiti hizi zote zinahitilafiana na utafiti wangu kwa kuwa hazikuwa na madhumuni ya kubainisha kuwa maudhui katika nyimbo hubadilikabadilika kadiri jamii inavyobadilika kila mara, huku

maudhui haya yakisawiri uhalisi wa historia ya wakati wake. Jamii ya Waembu imebadilika sana kijamii, kiuchumi, kisiasa na kidini tangu kipindi cha kabla ya ukoloni hadi sasa. Kwa hivyo, utafiti huu unalenga kudhihirisha kwamba mabadiliko haya yamesababisha kubadilika kwa maudhui katika nyimbo, swala linalotokea kiwakati. Nyimbo za harusi za jamii ya Waembu zitatumika kama mfano wa kuonyesha jinsi maudhui katika nyimbo yanavyobadilika kiwakati.

1.3 MASWALI YA UTAFITI

Tasnifu imejaribu kujibu maswali yafuatayo:

- i) Maudhui ya nyimbo za harusi za jamii ya Waembu kabla ya maingilio ya wakoloni yalikuwa yapi?
- ii) Maudhui ya nyimbo za harusi za jamii ya Waembu baada ya maingilio ya wakoloni yalikuwa yapi?
- iii) Mabadiliko haya ya maudhui yanaweza kuelezwa vipi kinadharia?
- iv) Mabadiliko haya ya maudhui yamechangiwa na matukio gani ya kijamii?

1.4 NADHARIA TETE

Utafiti huu umeongozwa na nadharia tete zifuatazo:

- i. Maudhui ya nyimbo kama utanzu wa fasihi simulizi husawiri mwelekeo wa jamii kuhusu maisha kwa jumla katika kipindi husika kwani nyimbo hizi huchota maudhui yake kutoka kwenye jamii.
- ii. Maudhui ya nyimbo kama utanzu wa fasihi simulizi husawiri uhalisi wa maisha ya jamii katika historia ya wakati wake.
- iii. Mabadiliko ya maudhui kiwakati katika utanzu wa nyimbo husababishwa na mabadiliko ya jamii kisiasa, kiuchumi, kidini pamoja na asasi zingine za jamii kwa jumla.

1.5 MALENGO YA UTAFITI

Malengo ya utafiti huu ni kuonyesha kwamba maudhui ya nyimbo za harusi miongoni mwa watu wa jamii ya Waembu yamebadilika tangu kabla ya maingilio ya wakoloni hadi hii leo (baada ya maingilio ya wakoloni). Aidha, utafiti huu umejaribu kuchunguza na kueleza matukio ya kijamii yaliyochangia mabadiliko haya. Licha ya hayo, utafiti huu umelenga kueleza mabadiliko haya ya maudhui kinadharia.

1.6 SABABU ZA KUCHAGUA MADA HII

Watafiti wengi wa fasihi simulizi wamefanya utafiti wa kina kuhusu maudhui katika utanzu wa nyimbo. Hata hivyo, tafiti hizi zimeshughulikia maudhui katika nyimbo kama kipengee cha kazi ya fasihi, huku wakipuuza ukweli kwamba maudhui katika nyimbo kama utanzu wa fasihi simulizi hubadilika na wakati kuambatana na mabadiliko yanayoikumba jamii, haswa tukielewa fika kwamba fasihi huchota maudhui yake katika jamii.

Nandwa na Bukenya (1983) wasema kuwa maudhui katika nyimbo zitekelezazo majukumu mbalimbali katika jamii hubadilika pindi mabadiliko ya kijamii yanapotokea.

Wa Thiong'o (1972: 6) asema kuwa fasihi haitokei katika ombwe tupu, inapewa mwelekeo, umbo na umuhimu wake na maswala ibuka katika jamii mahususi. Maswala yanayoipa fasihi mwelekeo ni ya kiuchumi, kijamii pamoja na kisiasa. Mabadiliko yatokeayo katika nyanja hizi huathiri kazi ya fasihi kwa jumla, maudhui yakiwemo.

Kutokana na haya, basi, utafiti huu unanuia kujaza pengo kutokana na tafiti za hapo awali ambazo zilishindwa kuonyesha kwamba maudhui ya nyimbo mbalimbali, haswa za harusi, hubadilika sambamba na mabadiliko ya maisha katika jamii.

Sababu nyingine ya kuchagua mada hii ni kuonyesha kwamba hakuna haja mgogoro uliopo baina ya vijana na wazee wanaoshiriki katika kuimba nyimbo zenye maudhui yenye mwelekeo tofauti. Vijana wa kisasa wanazipiku nyimbo za harusi za Kiambu zilizoimbwa kabla ya maingilio ya wakoloni kwa kusema kuwa zimepitwa na wakati, huku wazee wa enzi za ukoloni wakiona kuwa nyimbo za baada ya ukoloni haziendelezi maadili mema katika jamii. Utafiti huu unalenga kuonyesha kuwa maudhui ya nyimbo za harusi katika jamii ya Waambu hubadilika kiwakati sambamba na mabadiliko ya kijamii. Kutokana na haya, basi ni bayana kwamba nyimbo za baada ya ukoloni na kabla ya ukoloni zina dhima sawa katika utekelezaji wa majukumu ya nyimbo za harusi za jamii ya Waambu.

Mwisho, mada hii ina lengo la kuendeleza nadharia ya Graig (1975) kwamba matukio makuu ya mwongo fulani yaweza kutambulika kutokana na fasihi ya muongo huo, haswa tunapochunguza kipengele cha maudhui kwa vile ni “kioo cha jamii” na hubadilika kiwakati kadiri jamii inavyozidi kukumbwa na mabadiliko.

1.7 UPEO WA UTAFITI

Utafiti huu ulishughulikia mabadiliko ya maudhui kiwakati katika nyimbo za harusi za jamii ya Waembu tangu kabla ya maingilio ya wakoloni na baada ya maingilio ya wakoloni hadi hii leo. Utafiti huu ulishughulikia nyimbo kumi za kila mojawapo ya vipindi viwili vilivyoshughulikiwa pamoja na kuzitafsiri katika lugha ya Kiembu ili ziwakilishe nyimbo zote za harusi za kipindi husika.

1.8 MISINGI YA NADHARIA

Katika kutalii mabadiliko ya maudhui kiwakati katika nyimbo za harusi miongoni mwa jamii ya Waembu, mtafiti aliongozwa na nadharia mbili ambazo ni uhalisia na ufeministi wa Kiafrika.

Kulingana na Flaubert (1850) nadharia ya uhalisia huchambua au kueleza kazi ya fasihi kwa kutilia maanani maisha ya binadamu jinsi yalivyo katika uhalisi wake. Uhalisi huu unahusu uigaji wa mazingira anamopatikana mwanadamu. Hii ndiyo sababu inayoifanya nadharia hii kuwa mwafaka kutalii mabadiliko ya maudhui katika nyimbo za harusi za jamii ya Waembu, kwani maudhui haya hubadilika kufuatia athari za kiuchumi, kisiasa, kitamaduni na kijamii. Maudhui haya hubadilika kila wakati, huku yakisawiri uhalisi wa jamii hii. Msingi wa uhalisia ni kuielewa leo ya jamii kwa kutumia jana.

Nadharia ya ufeministi ni nadharia inayojishughulisha na utetezi wa wanawake dhidi ya ukandamizaji katika jamii iliyodhibitiwa na ubabedume. Nadharia hii huwa na misingi yake katika jamii, hasa majukumu yanayopewa wanawake na wanaume katika jamii. Kwa kifupi, nadharia hii huonyesha mwelekeo wa jamii kuhusu nafasi ya mwanamke katika jamii kwa jumla, ikiwa na nia ya kuondoa ubaguzi wa mwanamke kijinsia. Nadharia hii hujaribu kulete usawa katika nyanja zote maishani kati ya mwanamume na mwanamke.

1.8.1 NADHARIA YA UHALISIA

Kulingana na maoni ya Rene Wellek katika jarida lake la “Neophilogus”, XIV (1961.20) dhana ya uhalisia ilianza kutumika mnamo mwaka wa 1970 kumaanisha vitu thabiti vinavyohisika na mishipa ya fahamu ya binadamu pamoja na ukweli unaodhihirika katika kazi ya fasihi. Uhalisia wa kifasihi unaashiria uwezo wa kazi ya fasihi kusawiri au kueleza hali kwa kuzingatia uyakinifu au uhakika wa maisha. Kwa mujibu wa Flaubert (1850) uhalisia ni jinsi ya kueleza kazi ya sanaa kwa kutilia maanani maisha ya binadamu jinsi yalivyo katika uhalisia wake. Uhalisia huu unahusu uigaji wa mazingira anamopatikana mwanadamu. Kwa mujibu wa mwanafalsafa Hegel, katika kitabu chake *Aesthetics* uhalisia

unamaanisha kazi ya sanaa iliyo na wahusika ambao matendo yao yanachochewa na hali ya kisaikologia iliyowazunguka. Katika misingi ya uhalisia fasihi huchukuliwa kuwa “kioo cha jamii” kama anavyoeleza Wamitila (2002).

Qusby (1988) asema kwamba nadharia ya uhalisia ilianza kutumiwa kwa mara ya kwanza huko Ufaransa katika mwaka wa 1850 kueleza kazi za sanaa zilizojikita katika kuusawiri ulimwengu kama ulivyo, wala sio kama unavyofikiriwa kuwa. Kama nadharia ya uhakiki, uhalisia huzingatia namna ukweli unavyosawiriwa katika nyakati mbalimbali. Jinsi ya kuusawiri na kuuelewa uhalisia hutofautiana kutoka jamii moja hadi nyingine. Huu ndio msingi wa Qusby (1988) kwamba kila kizazi huwa na “uhalisia” wake na ndiyo sababu uhalisia katika kazi ya fasihi huwa ni swala la kijamaa.

Larkin (1972:2) anasema kuwa wanauhalisia waliamini kwamba madhumuni ya kazi ya fasihi ni kuwarudisha watu katika ulimwengu wao wa kawaida na kwamba ulimwengu unaoumbwa na kazi ya fasihi huwa na ukweli halisi wa wakati wake.

Lukacs (1972: 6) naye asema kwamba nadharia ya uhalisia ilianza kutumiwa katika kazi za fasihi kwani waasisi wa nadharia hii waliona

kwamba kuna uhusiano mkubwa kati ya kazi ya sanaa na mazingira halisi yanayozungumziwa.

Katika misingi hii, nadharia ya uhalisia inaweza kutumiwa kueleza mabadiliko ya maudhui katika nyimbo za harusi za jamii ya Waembu kutoka nyakati za kabla ya maingilio ya wakoloni wakati tamaduni za Waembu zilitawala katika jamii hii, baada ya maingilio ya wakoloni hadi hii leo haswa tunapozingatia mchango wa Graig (1975:134 - 160) “ matukio makuu ya mwongo fulani yaweza kutambulika kutokana na fasihi ya muongo huo. Matukio hayo hudhihirishwa na maudhui ya fasihi.” Wakitilia mawazo ya Graig nguvu, Wellek na Warren (1949:94 - 95) wasema kuwa fasihi ni taasisi ya kijamii inayotumia lugha, ni ubunifu wa kijamii. Vipengele vya fasihi kama maudhui, taswira na mdundo vinatokana na jamii. Historia ya jamii inapobadilika, maudhui hayo hubadilika.

Kufuatia ukweli uliotolewa na Graig (1975) pamoja na Wellek na Warren (1949) ni wazi kwamba nadharia ya uhalisia ina nafasi kubwa katika kutalii mabadiliko ya maudhui katika nyimbo za harusi za jamii ya Waembu kwani maudhui katika nyimbo hizi yalibadilika kufuatia mabadiliko yaliyoikumba jamii hii baada ya wakoloni kuingia katika

jamii hii na kuathiri asasi zake ndoa ikiwa baadhi ya asasi zilizopata athari hii.

Maoni ya Qusby (1988), Larkin (1972) na Lukacs (1972) kuhusu nadharia ya uhalisia vilevile yanaifanya nadharia hii kuweza kuongoza utafiti huu kwani wanafafanua kwamba kazi yoyote ya fasihi hubadilika na wakati kusadifu uhalisia wa jamii husika.

Mihimili ya Nadharia ya Uhalisia.

Nadharia hii ina mihimili mbalimbali ambayo mtumiaji hana budi kutilia maanani katika kufanya utafiti au kuihakiki kazi yoyote ya kifasihi.

Kwanza nadharia hii inashikilia kwamba hali zote za maisha ya kijamii huelezwa katika uhalisi wake kama unavyoonekana wala sivyo unavyofikiriwa kuwa. Uhalisia huu waweza kubadilika kufuatia mabadiliko ya hali mbalimbali za kijamii. Kufuatia ukweli huu, ni bayana kwamba nadharia ya uhalisia yaweza kutumika, kutalii mabadiliko ya maudhui ya nyimbo za harusi za jamii ya Waembu yaliyobadilika kufuatia mabadiliko ya hali mbalimbali za kijamii kama vile maingilio ya wakoloni yaliyobadili mielekeo ya maisha ya watu wa jamii hii. Huenda ikawa mabadiliko haya yalichangia katika kubadili maudhui ya kazi za fasihi kwa jumla. Kauli hii inapata nguvu haswa tunaporejelea mawazo ya Nandwa na Bukenya (1983) kuwa kazi ya fasihi haitokei katika

ombwe tupu bali huchota maudhui yake katika jamii. Mabadiliko ya mielekeo ya maisha huenda sambamba na mabadiliko ya maudhui katika kazi ya fasihi, haswa fasihi simulizi.

Muhimili mwingine muhimu wa nadharia ya uhalisia ni kwamba kazi za fasihi zinazotilia maanani matukio na mandhari ya kawaida na yanayoweza kupatikana katika jamii huthaminiwa zaidi kwa kuwa fasihi husawiri mielekeo ya watu katika jamii. Huu ndio msingi wa Lenin aliyenukuliwa na Wamitila (2002) kwamba fasihi ni “kioo cha jamii”.

Muhimili huu wa nadharia ya uhalisia utakuwa muhimu kueleza mkondo wa mabadiliko ya maudhui katika nyimbo za harusi za jamii ya Waembu.

Mwisho, nadharia ya uhalisia hushikilia kwamba mielekeo ya jamii haipingani na historia ya wakati wake. Hivi ni kusema kwamba historia ya jamii yoyote ile husawiri mwelekeo wake kuhusu maswala mbalimbali ya kijamii fasihi ikiwemo. Muhimili huu unaipa nadharia ya uhalisia uwezo mkubwa wa kuongoza utafiti wa mada hii, kwani itakuwa msingi imara wa kueleza jinsi mabadiliko ya maudhui katika nyimbo za harusi za jamii ya Waembu yalivyobadilika kufuatia mabadiliko ya historia ya jamii hii kutoka kipindi cha kabla ya maingilio ya ukoloni hadi hii leo.

Kwa hakika, muhimili wa nadharia ya uhalisia unaodhihirisha utendakazi wake waonyesha bayana kuwa nadharia yenyewe ni msingi imara wa kuongoza utafiti huu.

1.8.2. NADHARIA YA UFEMINISTI

Nadharia ya ufeministi iliasisiwa na Woolf, Ellman, Millet na De Beauvoir (1960).

Nadharia ya ufeministi ina misingi na mizizi yake katika nchi za Kimagharibi. Ilianza kutumika katika karne ya kumi na tisa kufuatia kunyanyaswa kwa mwanamke katika jamii zilizotawaliwa na itikadi kali za kiume. Kule Marekani, wafeministi wa kwanza walianza kuhusisha hali ya wanawake na hali mbalimbali za watumwa wa Kiafrika waliohudumia mabwana wa Kimarekani. Nadharia ya ufeministi hujihusisha na kupigania ukombozi wa mwanamke katika jamii.

Ruthven (1984:28) anamnukuu Marx akisema kuwa ukandamizwaji wa mwanamke ni swala linalotokana na uwezo wa kuzalisha mali pamoja na kumiliki mali hiyo. Marx aendelea kusema kwamba uzalishaji mali ndicho kitovu na chanzo cha matabaka ya kijamii na kuwa ndicho chanzo cha dhuluma zote. Marx hupendekeza kwamba dhuluma dhidi ya

wanawake zitaisha pale ambapo dhuluma dhidi ya wanyonge wote zitakapoisha.

Wafuasi wa mtazamo wa ki-feministi hawaafikiani na mtazamo huu wa Kimarx kuhusu kukombolewa kwa mwanamke, kwani utabaka sio jambo la kipekee lililochangia ukandamizwaji wa mwanamke. Eisenstein (1975:5) aeleza kwamba ukandamizwaji wa mwanamke na wanaume ulikuwepo hata kabla ya majilio ya mfumo wa kibepari. Eisensteni (1975) asema kwamba ukandamizwaji wa wanawake ni swala la kijamii na kiwango cha ukadamizwaji na udunishaji wa mwanamke hutofautiana katika misingi ya rangi, cheo, dini, kijamii kiuchumi na kadhalika. Katika misingi hii, wanaharakati walitofautisha ufeministi wa Kiafrika na ule wa Kimagharibi.

1.8.3 NADHARIA YA UFEMINISTI WA KIAFRIKA

Ufeministi wa Kiafrika unaangazia mwanamke katika mwelekeo wa Kiafrika, huku ule wa Kimagharibi ukiangazia ukandamizwaji wa mwanamke katika mwelekeo wa kimagharibi. Kwa kuwa utafiti huu uliangalia nyimbo za harusi katika jamii ya Kiafrika na jinsi maudhui katika nyimbo hizi yalivyomsawiri mwanamke, basi nadharia ya ufeministi mtazamo wa Kiafrika ilifaa zaidi kuongoza utafiti huu. Wafula R. M. na Kimani N. (2007) wasema kuwa ufeministi wa Kiafrika una

mihimili kadha wa kadha. Mihimili hii huonyesha jinsi jamii mbalimbali za Kiafrika zinavyomsawiri mwanamke.

Mihimili ya Ufeministi wa Kiafrika

Baadhi ya mihimili hii ni kusawazisha wanadamu kwa upande wa utamaduni na uana. Inapigania jamii mpya yenye misingi katika amali za kibinadamu bila kujali maumbile. Katika jamii nyingi za Kiafrika, wanawake wengi walibaguliwa kitamaduni na kiuana. Nyimbo za harusi za Kiembu ziiimsawiri mwanamke kama kitu hasi na kando, huku mwanamume akichukuliwa kama binadamu kielelezo. Ndoa ni asasi mojawapo ya kitamaduni inayoendeleza ukandamizwaji wa wanawake. Asasi yenyewe imejengwa kwenye imani ya uwezo mkubwa alionao mwanamume na kuishia kumwangalia mwanamke kama chombo tu. Mwelekeo huu huenda ukaathiri maudhui ya nyimbo za harusi katika jamii ambapo harusi ilitokelezwa kufuatia itikadi kali za kitamaduni kabla ya maingilio ya wakoloni kwani utamaduni wa Waembu kwa jumla haukuwa umepata athari za Wakaloni, dini ya kimagharibi ikiwa mojawapo ya athari hizi. Nyimbo za harusi zilizoimbwa zilidhihirisha maudhui fulani kuhusiana na mwelekeo wa jamii kuhusu nafasi ya mwanamke katika jamii. Jamii ilivyozidi kubadili mwelekeo kuhusu nafasi ya mwanamke katika jamii, ndivyo maudhui katika nyimbo hizi yalivyozidi kubadilika. Kutokana na ukweli huu basi nadharia ya

Ufeministi wa Kiafrika ni mwafaka katika utafiti huu kwani imetusaidia kubaini jinsi mwanamke anavyosawiriwa kupitia fasihi simulizi ya nyimbo miongoni mwa jamii ya Waembu katika vipindi mbalimbali vilivyoikumba jamii hii ambavyo kihistoria ni kabla ya maingilio ya wakoloni na baada ya maingilio ya wakoloni.

Nadharia ya ufeministi wa Kiafrika hutumia fasihi kama jukwaa la kueleza hali inayomkumba mwanamke katika jamii ya Kiafrika ili ieleweke na wengi. Nyimbo za harusi ni baadhi ya kazi za fasihi zinazoeleza hali inayomkumba mwanamke kupitia maudhui yanayopatikana katika nyimbo hizi. Katika misingi hii, nadharia hii ilifaa utafiti huu kwani ilisaidia kuchanganua maudhui katika nyimbo za harusi za jamii ya Waembu, kwani maudhui haya ni kielelezo cha hali zinazomkumba mwanamke katika jamii ya Kiafrika ambapo jamii ya Waembu ni mojawapo ya jamii hizi.

Nadharia ya ufeministi wa Kiafrika hujaribu kuamsha mwamko mioyoni mwa wanawake ili washiriki katika ukombozi wao. Baadhi ya nyimbo za harusi katika jamii ya Waembu, haswa za kabla ya maingilio ya wakoloni zilionyesha jinsi wanawake walivyotaribu kujikomboa kutokana na ukandamizwaji ulioendelezwa na wanaume. Katika misingi hii, nadharia hii ilifaa utafiti huu, kwani ilichangia kuyachanganua maudhui ya nyimbo

kama hizi ambayo yalidhihirisha ujumbe uliopitishwa na wanawake ulioangazia ukombozi wao.

Nadharia ya ufeministi wa Kiafrika inakuza na kuendeleza hisia za umoja wa wanawake kama kundi linalodhulumiwa. Muhimili huu umekuwa wenye manufaa katika utafiti huu haswa tukirejelea umoja uliodhihirika miongoni mwa wanawake wa jamii ya Waembu katika kuimba nyimbo za majigambo kujaribu kuzima dhuluma dhidi ya wanaume. Walijitenga kuimba nyimbo hizi baada ya kudhulumiwa na wanaume. Muhimili huu ni muhimu kwani umechangia katika uchambuzi wa maudhui katika nyimbo za harusi za jamii ya Waembu zilizoimbwa na wanawake pekee.

Nadharia ya ufeministi wa Kiafrika inajaribu kuhamasisha utungaji wa kazi za sanaa zenye wahusika wa kike wanaoweza kuigwa na wasiotegemea wanaume ili kujitambulisha. Muhimili huu umekuwa muhimu katika utafiti huu kwani umesaidia kuchambua maudhui yaliyomsawiri mwanamke kama shujaa, haswa kwa kuweza kuzaa mtoto msichana anayeitajirisha jamii kupitia mahari pamoja na kusababisha mkusanyiko wa vikao muhimu kama sherehe za ndoa na vya kuafikiana kuhusu mahari.

Nadharia hii ilikuwa msingi imara wa utafiti huu kwani ni msingi au kielelezo cha maswala ya wanawake kama mapenzi, ndoa, ukombozi wao

n.k. maudhui katika nyimbo za harusi za jamii ya Waembu huwa na mengi kuhusu maswala ya wanawake. Basi nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika yaingiliana pakubwa na mada ya utafiti.

1.9 YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA YA UTAFITI

Nandwa na Bukenya (1983) wasema kuwa utanzu wa fasihi simulizi, haswa ya Kiafrika, haujafanyiwa utafiti mwingi ukilinganishwa na fasihi andishi. Hii ndiyo sababu watafiti wengi katika uwanja huu wanapendekeza kwamba pana haja ya kufanya utafiti wa kina kusudi kufafanua maswala tata katika uwanja huu. Watafiti na wasomi wa fasihi simulizi ya Kiafrika kama vile King'ei na Kisovi (2002: 19-20) na Taban Lo Liyong kama anavyonukuliwa na Nandwa na Bukenya (1983: 39) wanadhihirisha kwamba pana haja ya kufanya utafiti wa kina katika fasihi simulizi ya Kiafrika kusudi kuikuza na kuihifadhi. Taban Lo Liyong anukuliwa na Nandwa na Bukenya (1983) akisema kuwa fasihi simulizi ya Kiafrika ni uga tasa. Sababu ya utasa huu ni kwamba hapajawa na utafiti wa kuridhisha uliofanyiwa uga huu kusudi kuukuza na kuuelewa zaidi.

King'ei na Kisovi (2005:19-20) nao wamechangia katika kuonyesha haja ya kufanya utafiti wa kina katika fasihi simulizi pale walipoorodhesha maswala muhimu kuhusu fasihi simulizi ambayo yapaswa kushughulikiwa.

Hata hivyo, pamekuwa na juhudi za kufanya utafiti katika fasihi simulizi huku miongoni mwa watafiti wa kwanza wa fasihi simulizi wakiwa Werner (1965), Siedel (1972), Valtan (1974), Mbaabu, (1978), na wengine.

Hawa walijikita zaidi katika kutafiti tanzu za ngano, vitendawili, hadithi na methali. Baada ya watafiti hawa kuonyesha ya kwamba pana haja ya kuifanyia fasihi simulizi utafiti wa kina, tafiti nyingi zilizofanywa zilishughulikia tanzu na vitanzu vya fasihi simulizi, pamoja na vipengele anuwai vya tanzu na vitanzu hivi, huku maudhui yakiwa mojawapo ya vipengele hivi.

Finnegan (1970) alifanya utafiti kuonyesha umuhimu wa nyimbo katika jamii za Kiafrika na jinsi dhima ya nyimbo hizi inavyobainika. Utafiti wa Finnegan uliweka wazi kwamba umuhimu au dhima ya nyimbo hupatikana kupitia maudhui na mtindo. Utafiti wa Finnegan ni muhimu kwa utafiti wangu, kwani ulihusu maudhui katika nyimbo. Hata hivyo, utafiti huu ulizua pengo kwa kukosa kubainisha kwamba maudhui katika nyimbo hubadilika na wakati kwa kuwa hali ya maisha katika jamii hubadilika kila uchao.

Chiuri (1984) alifanya utafiti kuhusu maudhui na fani ya nyimbo za Joseph Kamaru ambapo aligawa nyimbo hizi katika makundi kadhaa

kama mapenzi, siasa na jamii. Utafiti wa Chiuri ulifaa utafiti huu, kwani uligusia maudhui ya mapenzi katika nyimbo sawa na utafiti huu uliohusu maudhui katika nyimbo za harusi za jamii ya Waembu ambazo ni za kimapenzi. Hata hivyo, utafiti wa Chiuri ni tofauti na huu kwa kuwa ingawa uligusia maudhui ya mapenzi katika nyimbo, ulifanywa katika misingi ya mila na tamaduni za Wakikuyu, kinyume na huu uliofanywa katika misingi ya tamaduni za Waembu. Aidha utafiti huu haukushughulikia fani kama ule wa Chiuri.

Ndungo (1985) alitafiti kuhusu wanawake na mabadiliko ya kihistoria katika fasihi ya Kiswahili akiwa na lengo la kuangalia jinsi mwanamke alivyochorwa katika nyakati mbalimbali za historia, sababu za mwanamke kusawiriwa hivyo, pamoja na kupendekeza njia inayofaa ya kuwasawiri wanawake katika fasihi ya Kiswahili. Ili kutimiza malengo ya utafiti wake, Ndungo alilazimika kutalii maudhui yaliyoshamiri katika kazi mbalimbali za fasihi ya Kiswahili. Alimnukuu Magayu K. Magayu (1974:4) katika makala yake "The East African Literature and the East African Writer" aliyesema kuwa fasihi ni kielelezo cha hali halisi ya maisha. Kutokana na haya, msanii kama mwanajamii, huandika kutokana na tajriba anayoipata kutoka jamii anamoishi. Kazi nyingi za fasihi huweza kueleweka kupitia maudhui yake yanayohusu jamii na wakati fulani. Utafiti wa Ndungo ulifaa utafiti huu pakubwa kwa kuelekeza

kuelewa jinsi maudhui katika kazi yoyote ya fasihi yanavyojengeka. Hata hivyo, tafiti hizi mbili ni tofauti haswa tukizingatia malengo yake. Ndungo alitumia kipengele cha maudhui katika fasihi ya Kiswahili kubainisha mabadiliko ya kihistoria na wanawake katika fasihi hiyo. Huu nao ulitumia kipengele cha maudhui kuonyesha jinsi maudhui katika fasihi simulizi yanavyobadilika kiwakati. Nyimbo za harusi za jamii ya Waembu zimetumiwa kama data asilia.

Spencer (1985) asema kwamba nyimbo huwa na jukumu muhimu katika jamii, haswa za Kiafrika. Kuifahamisha jamii kuhusu mabadiliko yanayotokea maishani mtu anapozidi kukua ni mojawapo ya majukumu haya. Spencer aorodhesha mifano ya mabadiliko haya kama tohara, ndoa na mauti. Utafiti wa Spencer ulikuwa muhimu kwa utafiti huu kwani ulishughulikia nyimbo za ndoa sawa na huu. Hata hivyo, utafiti wa Spencer ni tofauti na huu, kwani alishughulikia maudhui katika nyimbo mbalimbali kuonyesha mabadiliko ya kijamii. Utafiti huu ulishughulikia mabadiliko ya maudhui kiwakati katika nyimbo za harusi za jamii ya Waembu na haukuwa na nia ya kuonyesha jinsi nyimbo zinavyobadili hali mbalimbali za maisha ya watu.

Mwaniki (1986) alifanya utafiti kuhusu tamaduni za Waembu ambapo nyimbo hutumika. Abainisha tamaduni hizi kama harusi, mazishi na

shughuli zote zinazohusiana na utaratibu wa ndoa. Utafiti wa Mwaniki ulinufaisha huu kwani ulielekeza kubaini nyimbo zinazotawala shughuli au utaratibu wa ndoa katika jamii ya Waembu, pamoja na kutalii maudhui yanayosheheni katika nyimbo hizi. Utafiti wa Mwaniki ni tofauti na huu kwani lengo lake lilikuwa kuonyesha tamaduni za Waembu ambapo nyimbo zilitumika. Lengo la utafiti huu lilikuwa kuonyesha kwamba maudhui ya nyimbo hubadilika kiwakati, wala si kuonyesha nyimbo zinazotumika katika tamaduni mbalimbali.

Ngugi (1988) asema kwamba nyimbo huwa zinathibitisha ubunifu wa mtu pamoja na uwezo wa kutumia akili yake kwa urazini. Nyimbo huonyesha maswala muhimu kuhusu jamii. Jukumu la nyimbo haswa ni kuielimisha jamii kupitia onyo, kuifahamisha pamoja na kuitahatharisha kuhusu hatari iliyoko maishani. Jukumu hili hutekelezwa kupitia maudhui yashirikishwayo katika nyimbo hizi. Utafiti wa Ngugi ni muhimu kwa utafiti huu kwani ulishughulikia maudhui katika nyimbo na hasa kuonyesha jinsi yanavyojengeka. Utafiti wa Ngugi ni tofauti na huu, kwani lengo lilikuwa kuonyesha jinsi maudhui katika nyimbo kwa jumla yanavyojengeka. Huu nao ulilenga kuonyesha jinsi maudhui ya nyimbo, haswa za harusi ya jamii ya Waembu, yanavyobadilika kiwakati.

Kabira na Karega (1988) walifanya utafiti kuhusu fasihi simulizi ya Wagikuyu ambapo walifafanua kwamba jukumu la wimbo kama utanzu wa fasihi simulizi hutegemea wakati au kipindi wimbo huo ulipoimbwa. Utafiti wa hawa ulikuwa na lengo la kuorodhesha nyimbo za jamii ya Wagikuyu zilizotekeleza majukumu mbalimbali katika jamii hiyo, ambapo walisema kwamba kulikuwa na nyimbo zilizotekeleza majukumu ya kuburudisha, kuonyesha mwelekeo wa jamii ya Wagikuyu kuhusu wanawake, kuonyesha historia ya watu pamoja na usanii wao. Utafiti wa wawili hawa uligusia maudhui wakiwa na lengo la kuchunguza iwapo wimbo ulifaa utendakazi wake katika kipindi husika cha jamii hii pasipo kuonyesha kwamba maudhui katika nyimbo hizi yalibadilika na wakati. Ingawa utafiti wa Kabira na Karega unafaa huu kwa kuelekeza kubainisha jinsi maudhui katika nyimbo yalivyochanganuliwa, tafiti hizi ni tofauti kwa kuwa Kabira na Karega hawakushughulikia jinsi maudhui katika nyimbo kama utanzu wa fasihi simulizi yanavyobadilika kiwakati.

Nkonge (1988) alitafiti fani na maudhui katika nyimbo za Joseph Kamaru ambapo alijaribu kuonyesha jinsi Kamaru anavyochota maudhui yake kutoka matukio ya kijamii na yale ya kisiasa nchini Kenya. Utafiti wa Nkonge ulikuwa na manufaa kwa utafiti huu kwani ulidhihirisha kwamba maudhui ya nyimbo huchotwa kutokana na matukio ya kijamii. Hata hivyo, utafiti wa Nkonge ni tofauti na huu kwani ulishughulikia uchoaji

wa maudhui ya nyimbo, ilhali huu ulishughulikia mabadiliko ya maudhui katika nyimbo kwa kutumia nyimbo za harusi za jamii ya Waembu kama mfano. Aidha nyimbo zilizoshughulikiwa na Nkonge ni za jamii ya Wakikuyu na zilizoshughulikiwa na utafiti huu ni za jamii ya Waembu.

Ntarangwi (1990) alifanya utafiti kuonyesha maudhui katika nyimbo za Remi Ogaro. Madhumuni yake ni kuonyesha jinsi maudhui ya utetezi yalivyojitokeza katika nyimbo za Ogaro na uhalisi wa maudhui hayo katika jamii za watu wa nchi za Afrika mashariki. Utafiti wa Ntarangwi ulifaa utafiti huu kwani ulidhihirisha kwamba maudhui ya wimbo huonyesha uhalisia wa kijamii katika historia ya wakati wake. Ukweli huu ulichangia kuonyesha kufaa kwa nadharia ya uhalisia iliyotumiwa kama nadharia msingi ya utafiti huu. Tofauti iliyoko baina ya utafiti wa Ntarangwi na huu ni kwamba wake ulishughulikia uhalisia wa maudhui ya nyimbo za Remi Ogaro katika jamii za watu wa nchi za Afrika Mashariki kwa jumla pasipo kuonyesha jinsi maudhui hayo yalivyobadilika kiwakati.

Yalwala (1991) alifanya utafiti kuhusu maudhui katika nyimbo za John Mwale ambapo alitathimini maudhui haya kwa kipimo cha muktadha ulizozizaa. Maudhui yaliyojadiliwa ni yale ya siasa, umoja, uzalendo na maadili katika jamii. Utafiti huu wa Yalwala ni muhimu kwa utafiti huu

kwani unasawiri wimbo kama zao la miktadha ya kijamii. Nyimbo hizi huibuka kufuatia utaratibu fulani ambao unachangiwa na maswala ibukizi katika jamii. Hiki ni kidokezo cha jinsi maudhui ya nyimbo za harusi za jamii ya Waembu yalivyobadilika kufuatia maswala yaliyotokea katika jamii hii kiwakati. Tofauti baina ya tafiti hizi mbili ni kwamba Yalwala alishughulikia nyimbo za aina mbalimbali akiwa na nia ya kuonyesha uhusiano uliopo baina ya maudhui katika wimbo na muktadha uliotungiwa. Lakini huu ulilenga kuonyesha mabadiliko ya maudhui katika nyimbo kiwakati.

Mbiti (1991: 7-8) asema kwamba nyimbo, methali, hekaya na hadithi zapatikana katika jamii nyingi za Kiafrika. Fani hizi huwa zinatokea katika kipindi mahususi na huwa na ujumbe bainifu. Aidha, huwa na maudhui maalum kuhusu nyanja fulani za maisha. Maoni ya Mbiti yalinufaisha utafiti huu kwani yalifafanua kuwa nyimbo hutokea kipindi mahususi na huwa na maudhui maalum kuhusu nyanja fulani za maisha ambazo hubadilika mara kwa mara. Ingawa Mbiti alishughulikia mabadiliko ya maudhui kiwakati, alijihusisha na utanzu wa methali, hadithi na hekaya. Kumbe huu ulishughulikia mabadiliko ya maudhui katika utanzu wa nyimbo kiwakati.

Chesaina (1991) asema kwamba nyimbo zinahusiana na harakati za kila siku za maisha ya binadamu, haswa katika jamii ya Kiafrika. Harakati hizi ni kama sherehe za kunywa pombe, harusi, mazishi na nyinginezo. Nyimbo huweka dhahiri na kueleza harakati hizi kupitia maudhui yapatikanayo kwazo. Utafiti wa Chesaina ulikuwa na manufaa kwa utafiti huu kwani alidokeza kwamba nyimbo huwa na maudhui anuwai kutegemea jopo lake. Na kwa hakika, nyimbo za harusi za jamii ya Waembu zinaweza kuwekwa katika jopo maalum ambapo maudhui yake yanaweza kuchanganuliwa. Utafiti wa Chesaina ni tofauti na huu, kwani lengo lake lilikuwa ni kuorodhesha nyimbo za jamii za Kiafrika kulingana na harakati za kijamii zinazozizaa akiwa na nia ya kuonyesha kwamba maudhui katika nyimbo hutegemea muktadha.

King'ei (1992) alifanya utafiti kuhusu umuhimu wa nyimbo za taarab nchini Kenya kati ya 1963 na 1990. Alichunguza utendakazi wa nyimbo hizo kwa kuzingatia lugha, utamaduni, mawasiliano pamoja na maudhui ya nyimbo hizi. Utafiti wa King'ei ulifaidi utafiti huu kwa kuongoza mtafiti kubaini mambo muhimu ya kuzingatia katika kugundua maudhui ya nyimbo ambalo ni zoezi muhimu katika utafiti huu. Utafiti wa King'ei ni tofauti na huu kwani ulishughulikia utendakazi wa nyimbo kwa kuzingatia maudhui, lugha, utamaduni na mawasiliano.

Mwai (1997) alitafiti kuhusu nguvu za nyimbo kwa wanawake Waswahili. Alibainisha kwamba ingawa wanaume wa jamii ya Waswahili wana uwezo uliokithiri katika ndoa, wanawake wamebuni njia zao za kuelezea hisia zao kama vile viashiria, maumivu na mateso kupitia nyimbo. Hisia hizi hudhihirika kupitia maudhui katika nyimbo hizi. Utafiti wa Mwai una manufaa sana, kwani ulishughulikia upitishaji wa hisia za mapenzi katika nyimbo za ndoa na jinsi hisia hizi zinavyojenga maudhui katika nyimbo hizi. Hata hivyo utafiti wa Mwai ni tofauti na huu, kwani lengo lake lilikuwa ni kuonyesha kwamba maudhui katika wimbo hujenga hisia za watu.

Kwa hakika, tafiti nyingi zimefanywa kuhusu maudhui katika nyimbo. Hata hivyo, hakuna utafiti uliofanywa kuonyesha kwamba maudhui katika nyimbo za harusi za jamii ya Waembu hubadilika na wakati. Utafiti huu unanua kuonyesha kwamba maudhui katika nyimbo hizi hubadilika kiwakati kusawiri uhalisi katika historia ya jamii husika.

1.10 MBINU ZA UTAFITI

1.10.1 Maktabani

Utafiti huu ulifanywa maktabani kwa kiasi kikubwa. Madhumuni ya kuufanyia utafiti huu maktabani yalikuwa ni kupata maelezo zaidi kuhusu nadharia ya uhalisia na ile ya ufeministi wa Kiafrika, kwani ndizo

zilizotumika katika utafiti huu. Aidha, mtafiti alitumia maktaba kusudi kujifahamisha kwa kina yaliyoandikwa kuhusu mada ya utafiti, pamoja na kupata habari muhimu kuhusu mada ya utafiti, haswa tukitilia maanani kwamba uandishi ni mojawapo ya njia za kuhifadhi fasihi simulizi. Maandishi kuhusu fasihi simulizi ya Waembu, haswa utanzu wa nyimbo yalisomwa. Maktaba za vyuo vikuu vya Kenyatta, Nairobi na Chuo kikuu cha Kikatoliki cha Afrika Mashariki na kati zilitumiwa katika utafiti huu.

1.10.2 Nyanjani

Utafiti huu ulifanyiwa katika wilaya ya Embu ambapo kata tano zilichaguliwa, huku kata moja ikichaguliwa kutoka kila Tarafa. Kata ya Nembure ilichaguliwa kutoka Tarafa ya Nembure, Kigaa kutoka Runyenjes, Mufu kutoka Kyeni, Kigari kutoka Tarafa ya Manyatta na Iveche kutoka Tarafa ya "Central" (Kati). Masogora wawili wa nyimbo za jadi za harusi ya jamii ya Waembu walichaguliwa kutoka kila kata, walihojiwa na, hatimaye kuombwa kuimba nyimbo za jadi za harusi miongoni mwa watu wa jamii ya Waembu. Kigezo cha umri kilitumiwa kuchagua wahojiwa, ambapo waliochaguliwa walikuwa wale wenye umri wa miaka sabini na zaidi, haswa walioshiriki katika uimbaji wa nyimbo za harusi za kabla ya maingilio ya wakoloni.

Kwaya ya kanisa Katoliki ya Karingari ilichangia katika uimbaji wa nyimbo mbili za harusi katika jamii ya Waembu za baada ya maingilio ya wakoloni, kikundi cha akina mama cha *Murugi* kikashiriki katika uimbaji wa nyimbo, ambapo tano zilichaguliwa. Hatimaye, mtafiti alikusanya nyimbo tatu katika harusi ya Justa Muthoni na Kinyua Nthambiri, na Sally Munyi na Carol Murugi. Harusi hizi zilifanywa tarehe 24/11/07 katika kijiji cha Kirigiri na Rung'ang'a.

1.11 SAMPULI

Nyimbo kumi za harusi za jamii ya Waembu za kabla ya maingilio ya wakoloni zilikusanywa na kurekodiwa kwa lugha ya Kiembu. Baada ya hayo, nyimbo hizi zilitafsiriwa kwa Kiswahili.

Nyimbo zilizochanganuliwa ni zile zenye maudhui yaangaziayo maswala muhimu katika jamii ya Waembu kama vile maadili mema katika jamii, ushirikiano, thamani ya ndoa, thamani ya mali, nafasi ya mwanamke katika jamii n.k. Nyimbo hizi zilikuwa kiwakilishi tosha cha maudhui katika nyimbo za harusi za kabla ya maingilio ya wakoloni. Aidha, kata tano pekee ndizo zilizohusishwa katika ukusanyaji wa data, kwani ziliwakilisha wilaya ya Embu kikamilifu.

Baada ya kurekodi nyimbo za kabla ya maingilio ya wakoloni, mtafiti alirekodi nyimbo kumi za harusi ya jamii ya Waembu za baada ya maingilio ya wakoloni na kuzitafsiri kwa Kiswahili. Nyimbo zilizochaguliwa ni zile ambazo ziliwasilisha maudhui ya usawa kati ya mke na mume, zenye kuzungumzia mapenzi hadharani, zenye kufuata maadili ya dini, n.k. Sababu ya kuchagua nyimbo hizi ni kwamba ziliwakilisha mabadiliko ya maudhui katika nyimbo za harusi ya jamii ya Waembu kikamilifu.

1.12 MBINU ZA KUKUSANYA DATA

Mtafiti alitumia kanda za kunasa sauti kuhifadhi nyimbo hizi, pamoja na kamera kusudi kuhifadhi miondoko ya fanani, kwani huchangia katika ujenzi wa maudhui katika fasihi simulizi. Baada ya haya, mtafiti aliandika maneno ya nyimbo hizi kwa Kiembu, kisha kutafsiriwa kwa Kiswahili.

1.13 MBINU ZA UCHANGANUZI WA DATA

Data iliyotumika katika utafiti huu ilichanganuliwa kama ifuatavyo:

Nyimbo za harusi za jamii ya Waembu za kabla ya maingilio ya wakoloni ziliorodheshwa kwa Kiembu, kutafsiriwa kwa Kiswahili kisha baadaye maudhui yake yakaorodheshwa. Baada ya haya, nyimbo za harusi za jamii ya Waembu za baada ya maingilio ya wakoloni nazo

zilorodheshwa kwa Kiembu vilevile na kutafsiriwa kwa Kiswahili na baadaye maudhui yake yakaorodheshwa.

1.14 UWASILISHAJI WA MATOKEO

Baada ya kuorodhesha maudhui ya nyimbo za harusi za jamii ya Waembu za kabla na baada ya maingilio ya wakoloni, maudhui haya yalilinganishwa na kuelezwa kinadharia. Ilibainika kwamba maudhui yalibadilika na wakati, ingawa baadhi ya maudhui yaliendelea. Matokeo ya utafiti huu yalielezwa kikamilifu katika sura ya mwisho ya tasnifu.

1.15 HITIMISHO

Baada ya kupitia mambo ya kimsingi kuhusiana na tasnifu hii katika sura hii, sura ya pili inashughulikia nyimbo za harusi za jamii ya Waembu kabla ya maingilio ya wakoloni pamoja na kuchanganua maudhui ya nyimbo hizi.

SURA YA PILI

2.0 UTANGULIZI

Lengo kuu la sura hii ni kuorodhesha nyimbo za harusi za jamii ya Waembu za kabla ya maingilio ya wakoloni, pamoja na kuchanganua maudhui ya nyimbo hizi. Nyimbo hizi zimeorodheshwa katika makundi mawili makuu ambayo ni zile za wakati wa sherehe ya harusi yenyewe na za baada ya sherehe hiyo. Kwanza nyimbo hizi zilitolewa kwa lugha ya Kiembu, kisha kutafsiriwa kwa Kiswahili.

Mwaniki (1986:83-85) asema kwamba nyimbo zilitawala ndoa za jamii ya Waembu wakati wa sherehe ya harusi yenyewe, hadi baadaye wakati wa kumkaribisha mke nyumbani kwa mumewe na, hatimaye, wakati wa kusherehekea mahari iliyotolewa.

2.1 MAUDHUI KATIKA NYIMBO ZA WAKATI WA SHEREHE YA HARUSI

Ndungo (1985) alimnukuu Magayu K. Magayu (1974:4) katika makala yake "The East African Literature and East African Writer" aliyesema kuwa fasihi ni kielelezo cha hali halisi ya maisha. Kutokana na haya, msanii basi kama mwanajamii huandika au kusimulia kutokana na tajriba

anayoipata kutoka jamii anamoishi. Kazi nyingi za fasihi huweza kueleweka kupitia maudhui yake yanayohusu jamii na wakati fulani.

Katika misingi hii, maudhui ya nyimbo za harusi za jamii ya Waembu za wakati wa sherehe ya harusi yalichanganuliwa. Maudhui yaliyoshamiri katika nyimbo hizi ni maadili mema katika jamii, ushirikiano wa kijamii, ubaguzi wa wanawake kijinsia, pamoja na majigambo ya mwanamke kwa ule uwezo wake wa kuzaa, haswa watoto wasichana. Maudhui haya yalipatikana kupitia nyimbo nyingi zilizoimbwa. Ifuatayo ni mifano ya nyimbo zinazoshirikisha maudhui yaliyotajwa.

2.1.1 Mungariragia

Mukui: Li mungariragia-i

Etikia: Li mungariragia-i

Mukui: Muviki wa mburi cietu-i

Etikia: Li mungariragia

Mukui: kwa murume ti kwa nyukwe-i

Etikia: Li mungariragia

Mukui: Nvevo y'otuku ndiriringi-i

Etikia: Li mungariragia

Tafsiri kwa Kiswahili

Furaha ya ndoa

Kiongozi: Naam! furaha ya ndoa

Kiitikio: Naam! furaha ya ndoa

Kiongozi: Bibi harusi mwenye kutupatia mbuzi

Kiitikio: Naam! Furaha ya ndoa

Kiongozi: Kwa bwanako si kwa mamako

Kiitikio: Naam! Furaha ya ndoa

Kiongozi: Baridi ya usiku haipo tena

Kiitikio: Naam! Furaha ya ndoa

Uliimbwa wakati wa kuwafanyia Bwana na Bi harusi tambiko za kitamaduni kusudi wakubalike kijamii kama mke na mume.

Wimbo huu waeleza furaha baina ya wapenzi wawili wakumbatianapo. Hii ndiyo haswa maana ya neno "*mungariragia*" (Kukumbatiana). Aidha, waeleza furaha ya familia ya msichana aliyeolewa baada ya kupata mbuzi na ile ya familia ya mvulana aliyepata mke. Bi harusi alishauriwa kuwa na mienendo mizuri baada ya kuwa mke, tofauti na alivyokuwa hapo awali, kwani kwa mumewe si kwa mamake. Mume pia alikumbushwa kwamba atapata joto kwa kuwa na mshirika wa karibu.

Wimbo huu unasheheni maudhui ya maadili mema katika jamii, haswa pale unapomshauri mke kuwa na mienendo mizuri, kinyume na alivyokuwa kabla ya kuolewa, kwani kwa mumewe si kama kwa mamake ambapo pengine alitenda lolote alilotaka. Alishauriwa kumtii mumewe. Aidha, maudhui ya Ushirika maishani yanadhihirika kutokana na wazo kwamba mume na mkewe watapata joto na hapana baridi tena. "Joto" hapa latumiwa kijazanda likimaanisha ushirika maishani. Maudhui katika wimbo huu yaweza kuelezwa na kuchanganuliwa katika misingi ya nadharia ya ufeministi wa Kiafrika, haswa tukizingatia swala la mke katika jamii ya Kiafrika ambapo apaswa kunyenyekea kwa mumewe pamoja na kumfurahisha. Huu ndio uliokuwa uhalisi wa maisha wa wakati huo unaoweza kuchanganuliwa katika misingi ya nadharia ya

uhalisia. Aidha, wimbo huu waonyesha mwelekeo wa jamii ya Waembu wa wakati huo kuhusu nafasi ya mwanamke katika jamii. Mwelekeo huu unadhihirisha uhalisi wa maisha katika jamii ya Waembu wakati huo ambao waweza kuchanganuliwa na kuelezwa katika misingi ya nadharia ya uhalisia iliyoongoza utafiti huu. Kwa mujibu wa nadharia hii, maswala ya kijamii kama nyimbo huonyesha uhalisi wa kijamaa katika kipindi husika.

Mwimbaji : Runji Kubuta

Umri: 86

Tarafa: Nembure

Lokesheni: Gaturi South

Kata : Nembure

Tarehe : 10/10/07

2.1.2 Ningundue ikivituka

*Uiu ningunda wa ngunde,
Uuki ni wa mwana tikwa uri wa wira
Ningundue ukivituka,
Yaya kuri arume yaya magambori.
Ningundue kana nyimwe
Uuki uyu ni wau?
Ni wa muka uria,
Uramukagia murume
Macarie kiria andu ao makaria*

*Ni ngundue kananyimwe,
Uuki ni wa mwana tikwa uri wa mugunda
Ni wa karugamano ko'riri
Ni wa kirinyaga gitaraga riua,
Ni kiara naku ni mwigunyi wa ng'ombe?*

Tafsiri kwa Kiswahili

Nipewe pombe ikipita

Nipewe pombe ninywe na nisipitishwe
Pombe hii si malipo ya kufanya kazi shambani
Haikupatikana kufuatia kufanyiwa kazi
Na yeyote pale shambani.

Nipewe kabla haijawafikia wanaume wasioiwachilia
Nipewe au ninyimwe

Pombe hii ni ya nani?
Ni ya mke atekelezaye majukumu ya kiuana
Kama kuzaa na kulea watoto
Nipewe pombe hii kwani imetokana na kazi ya kitandani

Wimbo huu uliimbwa wakati wa sherehe ya harusi watu walipokunywa pombe baada ya Bwana na Bi harusi kukubalika kuwa mke na mume baada ya kufanyiwa matambiko ya kitamaduni kwa mujibu wa jamii ya Waembu. Yeyote aliyekuwa ameolewa au kuoja alikuwa na haki ya kuinywa pombe hii. Hata hivyo, wanaume walifikiria kwamba wana haki ya kuinywa pombe hiyo zaidi ya wanawake, ndipo wanawake wakaanza kulalamikia ubaguzi huu wa kijinsia wakati wa kuinywa. Pombe hii, ilitiwa katika chungu kimoja na kuchotwa kwa upembe wa ng'ombe. Pombe hii ilipitishwa kutoka kwa mtu mmoja kwenda kwa mwingine kwa kutumia upembe ule ule.

Wimbo huu unadhihirisha maudhui ya ubaguzi wa kijinsia ambapo wanaume waliona kwamba wana haki ya kuinywa pombe kuliko wanawake. Hii ndiyo sababu wanawake wanapomba kupewa pombe kabla haijawafikia wanaume kwani waume wakishaipata, basi wanawake hawataionja asilani. Hili laonyesha mwelekeo wa jamii kuhusu mwanamke nyakati hizo. Mwisho, wimbo huu waonyesha maudhui ya majigambo ya mwanamke kufuatia uwezo wake wa kuzaa wasichana, swala linalosababisha kuwepo sherehe za unywaji wa pombe. Majigambo haya ni dhahiri kufuatia kauli ya mwanamke aombapo pombe na kusema “Nipewe pombe ama ninyimwe, pombe hii ni kutokana na juhudi zangu za kuzaa, si malipo kwa ajiri, ya kufanya kazi ya sulubu shambani inayoweza kufanywa na yeyote”. Nadharia ya uhalisia imetumika kuchanganua maudhui katika wimbo huu, haswa ya ushirika katika jamii. Ushirika wa wote ulidhaminiwa sana katika jamii ya Waembu ya wakati huo. Nadharia ya ufeministi wa Kiafrika imefaa sana kuchanganua maudhui ya majigambo ya mwanamke ambayo yanadhihirisha hisia za umoja wa wanawake kama kundi linalothulumwa katika jamii. Aidha, nadharia ya ufeministi wa Kiafrika yaweza kutumiwa kuchanganua maudhui ya ubaguzi wa wanawake katika misingi ya uana ambapo tamaduni za jadi za Kiafrika zilimbagua mwanamke.

Mwimbaji : George Sogoria
Umri: 96
Tarafa: Manyatta
Lokesheni: Ngandori
Kata : Kigari
Tarehe : 13/10/07

2.1.3 Kanya nduke twinuke

*Li kanya, I kanya nduke twinuke
Kana kanya uraraga mageniiri
Li kanya?
Kanyanya muthoni ngundagirua kuthia
Na kuvia njara tukivuta riiko-i
Kanya
Li kanya, ii kanya nduke twinuke
Kana kanya uraraga ugeniri-i
Kanya?
Ui iia kigaru kia vuurwa
Kanyanya muthoni kigaru kiavuuruwa
Muka uri ngoro aringwe ni gatetemo
Utari ngoro avinge nyomba amame, i kanya
I kanya, i kanya nduke twinuke
Kana kanya uraraga mageniiri-i
Kanya!*

Tafsiri kwa Kiswahili

-Kibuyu twende nyumbani

Kibuyu, kibuyu njoo twende nyumbani
Ama wewe hulala ugenini ulipoalikwa?
Wazazi wa mvulana aliytoa mtoto wangu,
Mimi hupewa pombe kwani pia
Naweza kutengeneza yangu ikanywewa.
Kibuyu, kibuyu njoo twende nyumbani
Ama wewe hulala ugenini ulipoalikwa
Mbio ya mgambo imepigwa, kibuyu twende nyumbani
Mwanamke aliyeonea sherehe zetu wivu ajinyonge
Mwanamke asiyeona wivu kwa ufanisi
Wetu afunge nyumba na alale
Na mumewe kusudi apate wake
Mwari aweze kusherehekea kama sisi

Kibuyu, kibuyu, twende nyumbani
Au wewe hulala ugenini?

Wimbo huu uliimbwa wakati sherehe za harusi zilipokaribia mwisho. Kibuyu kinachozungumziwa hapa ni kilichotumika kuibeba pombe iliyotumiwa kwenye sherehe za harusi. Kibuyu hiki kinashauriwa kukumbuka kurudi nyumbani baada ya sherehe zozote zile, wala si kulala ugenini. Hili ni fumbo lililotumiwa kumshauri Bi na Bwana harusi kuwa watu wenye msimamo maishani na si kuvutiwa na lolote waonalo maishani hadi kusahau wajibu wao kama mke na mume. Ikiwa mume na mke wangevutiwa na kulala ugenini kila mara, basi hawangeweza kujenga jamii yenye maadili mema.

Wimbo huu pia ulisisitiza umuhimu wa kuoia kusudi kupata watoto kuendeleza kizazi cha jamii pamoja na kuilinda dhidi ya maadui. Hii ndiyo sababu mke na mme wanashauriwa kuhakikisha kwamba wamelala pamoja nyumbani kwao kila mara.

Wimbo huu unasheheni maudhui ya maadili mema katika jamii ya Waembu. Unazungumzia mambo yaliyopigwa marufuku katika jamii hii ambayo maharusi hawapaswi kujihusisha nayo kusudi kujenga jamii kielelezo. Kwa muhtasari, maadili mema ni kama ushirika katika ndoa baina ya mke na mume, wajibu wa mke na mume katika ndoa na kuwa na msimamo thabiti kuilinda jamii pamoja na kuhifadhi maadili mema

katika jamii. Maudhui katika wimbo huu yamechanganuliwa katika misingi ya nadharia ya ufeministi wa Kiafrika uliogawa majukumu ya mke na mume kiuana. Maudhui ya maadili mema ya kijamii katika wimbo huu yamechanganuliwa katika misingi ya nadharia ya uhalisia ambayo imedhihirisha uhalisi wa maisha ya wakati huo kwa kuonyesha maadili yaliyodhaminiwa pamoja na mambo yaliyopigwa marufuku katika jamii ya wakati huo.

Mwimbaji : Kamwere Kubuta

Umri: 82

Tarafa: Manyatta

Lokesheni: Ngandori

Kata : Kigari

Tarehe : 13/10/07

2.2 MAUDHUI KATIKA NYIMBO ZA BAADA YA HARUSI

Nkonge (1988) asema kuwa maudhui ya nyimbo hutokana na matukio ya kijamii. Nyimbo za kipindi kimoja hushirikisha maudhui yanayofanana. Kauli ya Nkonge yaangazia sababu ya mfanano wa maudhui ya nyimbo za baada ya harusi, kwani ingawa zilipewa nyakati tofauti, zilipatikana katika kipindi kimoja cha kabla ya maingilio ya ukoloni.

Maudhui yaliyopatikana katika nyimbo hizi haswa ni maadili mema katika jamii, ushirikiano wa kijamii, ujasiri wa mwanamke, thamani kubwa iliyopewa ndoa, furaha katika ndoa, dhuluma dhidi ya wanawake

na thamani kubwa iliyopewa utajiri katika jamii. Ifuatayo ni mifano ya nyimbo zinazoonyesha maudhui yaliyotajwa hapa juu.

2.2.1 Muviki cenji

*Aia-i muviki cenji muviki cenji-
Li ui muviki cenji,
Nyama iri 'tara 'ronirue niu-i,
Ui muviki cenji!
Cenji! Cenji! Cenji!*

Tafsiri kwa Kiswahili

Bi harusi mjinga

Bi harusi mjinga! Bi harusi mjinga!

Ndiyo, Bi harusi mjinga!

Wawezaje kuona nyama ikiwa kwenye dari ya nyumba ya Bwana harusi?

Hata kwenye dari ya nyumba ya mama wa mume wako?

Yafunike macho yako!

Uliimbwa kumpokea Bi harusi kwa mumewe jioni ya siku ya kwanza katika ndoa.

Wimbo huu wamueleza bibi harusi ajifanyaye kuelewa zaidi mazingira mapya ya mumewe na kumwona mamake mumewe kuwa mjinga. Aidha, wimbo huu unampiku Bi arusi apekuayepekuaye kila kitu katika nyumba ya mumewe na ile ya mamaye mumewe na kumwita mjinga na mlafi. Kuona hadi kwenye dari ya nyumba ya mumewe na ya mamaye hiyo siku ya kwanza baada ya kuolewa limetumiwa kama fumbo kumaanisha ulafi.

Maudhui yadhahirikayo katika wimbo huu ni maadili mema katika ndoa. Maudhui haya yanaonekana kufuatia onyo dhidi ya Bi harusi kutopekua na kutaka kuona hata nyama iliyofichwa kwenye dari ya nyumba ya bwanake na ile ya mamake mumewe. Yanayobainika hapa ni kwamba nyimbo za harusi za jamii ya Waembu zilidhihirisha maudhui ya maadili mema katika jamii ya mke na mume wapatao katika ndoa. Onyo dhidi ya ulafi ni kiwakilishi cha thamani iliyopewa maadili mema katika jamii. Nadharia ya uhalisia imetumika kuchanganua maudhui katika wimbo huu kwa kuwa maudhui ya maadili mema yaliyomo katika wimbo huu yadhahirisha uhalisi wa maisha katika jamii ya Waembu ya wakati huo. Jamii hii iliweka thamani kubwa sana katika maadili mema miongoni mwa wanajamii.

Mwimbaji : Ileri Mathenge

Umri: 72

Tarafa: Kyeni

Lokesheni: Kagaari

Kata : Mufu

Tarehe : 15/10/07

2.2.2 Kunguira Mugeni

Mukui: Kungu-i

Etikia: Kunguira mugeni

Mukui: Kungu-i

Etikia: Kunguira mugeni

Wavaraca menuke na ngaatho

Kungu-i, kunguira mugeni

Tafsiri kwa Kiswahili

Shangilia mgeni

Kiongozi: Shangilia
Kiitikio: Shangilia mgeni
Kiongozi: Shangilia
Kiitikio: Shangilia mgeni kutoka mbali atakaporudi
kwao atushukuru shangwe mgeni.
Shangwe! Shangwe mgeni.

Wimbo huu uliimbwa baada ya sherehe za harusi ya kitamaduni miongoni mwa watu wa jamii ya Waembu. Ulikuwa na jukumu la kuwasindikiza wageni waliohudhuria harusi hiyo. Wimbo huu ulipoimbwa watu wote walishikana mikono. Ilikuwa ni lazima kwa jamii ya Bi harusi na ile ya Bwana harusi kushiriki katika wimbo huu.

Wimbo huu ulisheheni maudhui ya ushirika baina ya bwana na bibi harusi, baina ya familia ya bwana na bibi harusi na jamii kwa jumla. Kushikana mikono ni ishara ya ushirika katika ujenzi wa jamii kwa jumla. Maudhui ya ushirika yalionyesha uhalisi wa maisha katika jamii ya wakati huo. Basi nadharia ya uhalisia imetumika kuchanganua maudhui katika wimbo huu.

Mwimbaji : Kiringa Rurii

Umri: 75

Tarafa: Kyeni

Lokesheni: Kathanjuri

Kata : Kathari

Tarehe : 15/10/07

2.2.3 *Kanyanya Ngutindike*

*Kanyanya ngutindike
Umbirire muthoni niandetere
Nthenge iri mariethe
Yakuria maguta nginevaka ciero niigutura
Ngiciara mwana uyu, arume ni mwethithite
Mutanegua ngicaika.*

Tafsiri kwa Kiswahili

Nikutume mzazi wa mvulana aliyeoa msichana wangu

Nikutume mzazi
Umwambia aliyeoa msichana wangu,
Aniletee beberu aliyenona
Nile nyama kisha nijipake mafuta mapajani
Nitulize maumivu niliyopata nilipokuwa
Namzaa mwana huyu aliyeolewa na mwanao
Nilipomzaa mwana huyu, waume walikuwa wamejificha,
Wasisikie nikisononeka.

Uliimbwa kushurutisha mume kutoa mahari baada ya ndoa iwapo alichelea kufanya hivyo. Katika wimbo huu, mama wa msichana aliyeolewa anatumana kwa mvulana aliyemwoa mwanawe amletee beberu aliyenona, amle kisha alijipake mafuta kwenye mapaja yake ili ajiliwaze kufuatia maumivu makali aliyopata alipomzaa mwanawe wakati mumewe na waume wengine walipokuwa wamejificha wasisikie akisononeka kwa maumivu makali.

Maudhui ya wimbo huu ni ujasiri wa mwanamke, haswa kwa kuvumilia uchungu wa uzazi na kupuuzwa kwa mwanamke katika jamii ya kitamaduni ya Waembu.

Wanaume walimwacha mke wakati alipowahitaji zaidi kama wakati wa shughuli ya uzazi. Kwa kuweza kujifungua pasipo kusaidiwa na mume, mke ajisifu na kujiona kama shujaa na hata kuwa na majigambo. Maudhui katika wimbo huu yamechanganuliwa katika misingi ya nadharia ya ufeministi wa Kiafrika, haswa tukizingatia mhimili wake kwamba kazi za sanaa ya Kiafrika zapaswa kuwa na wahusika wa kike wanaoweza kuigwa na wasiotegemea wanaume ili kujitambulisha.

Mwimbaji : Mbaka Njue
Umri: 78
Tarafa: Runyenjes
Lokesheni: Kagaari
Kata : Kigaa
Tarehe : 15/10/07

2.2.4 Ngururi

Andu a muviki

Guku ni kwau x 2

Guku athoni makuyanika

Ta mwere wanikitwe wa gukima njovi.

Makigucagia ta mukua ukivia?

Niwikagaatia ugicererwa? X2

Na wauka na kanya kanini kairu!

Kanya kanini kairu!

Ta gagutava mai ma kuruga njovi!

Ni wikaga atia ugicererwa?

Andu a muvikania

Ni mburi na ng'ombe nguthaikaga

Nanie ni njau nguthaikaga,

Nie mukua gitonga kinene

Kai mutari indo ta ino?

Tafsiri kwa Kiswahili

Majibizano

Familia ya bibi harusi

Huku ni kwa nani x2

Huku wazazi na watu wa Bwana harusi

Wanajitandaza kama mawele ili kukauka kusudi kutumiwa kutengeneza pombe?

Huku ni kwa nani? Ambapo watu wa bwana harusi wanajikokota hivyo, pasipo kujali wakati.

Familia ya bwana harusi

Nilikuwa nikishughulikia mbuzi na ngo'ombe

Na mimi nilishughulikia ndama, mimi ni mke wa tajiri mkubwa

Kwani nyinyi hamna mali kama hii?

Wimbo huu uliimbwa katika kikao cha kujadili mahari ambayo ingetolewa katika ndoa. Ni wimbo wa malalamiko kwa sababu ya wazazi wa Bwana harusi kuchelewa kufika katika kikao ingawa walitarajiwa kuwa wa kwanza.

Katika wimbo huu wa majibizano, familia ya Bi harusi yalalamika kwamba watu wa upande wa Bwana harusi wamechelewa kuhudhuria sherehe ya ndoa. Wale wa familia ya Bwana harusi wajibu kwamba wamechelewa wakitunza mifugo yao, kwani wao ni matajiri. Hii ni ishara kwamba upande wa Bibi harusi ni masikini kwani hawana mifugo ya kutunza ndiyo maana wakafika shereheni mapema hivyo.

Wimbo huu unadhihirisha maudhui ya ushirikiano baina ya jamii hizi mbili unadhihirishwa na majibizano haya, huku kila upande ukichukua nafasi yake. Maharusi watakiwa kuwa na ushirika kama huu. Aidha, wimbo huu waashiria umuhimu mkubwa wa utajiri wa kijamii ulio msingi imara wa kudhibiti ndoa. Maharusi walishauriwa kuwa na ng'ombe na mbuzi wa kushughulikia. Maharusi walishauriwa kuwa wenye bidii na kutumia muda wao vizuri. Uhalisia ni nadharia ambayo imetumiwa kuchanganua maudhui ya ushirikiano na thamani iliyopewa utajiri wa mali, kwani huu ndio uliokuwa uhalisi wa maisha. Mifugo walikuwa kigezo cha kupimia utajiri wa mtu nyakati hizo.

Mwimbaji : Ciumwari Kagereki

Umri: 79

Tarafa: Runyenjes

Lokesheni: Kagaari

Kata : Ngeniari

Tarehe : 17/10/07

2.2.5 *Ndinegua mukiurania*

Ndinegua mukiurania x2

Ngina'wa "gicoco" niaca

Kuri ki?

Ndinegua mukiurania x 2

Ndinegua mukiurania x2

Ng'ina wa "njura ndune"

Niaca kuria ki?

Ndinegua mukiurania x2

Tafsiri kwa Kiswahili

Sikusikia mukiulizana

Sikusikia mukiulizana x2
Mamake “gicoco” atakula nini?
Sikusikia mukiulizana x2
Mamake “njura ndune”
Atakula nini?
Sikusikia mukiulizana x2

Wimbo huu uliimbwa na wanawake baada ya sherehe ya harusi kuwakejeli wanaume kwa kutowajali wake zao mara nyingi. Ulikuwa na majukumu ya kiuana ambapo Bwana harusi alitahadharishwa dhidi ya kumpuuza mke wake au kutojali atakula nini kama yalivyokuwa mazoea ya wanaume wazembe.

Mama “*Gicoco*” na mama “*Njura ndune*” ni majina yaliyochukuliwa kuwakilisha wanawake wote katika jamii ya Waembu.

Wimbo huu unadhihirisha maudhui ya maadili mema katika jamii ambapo mume apaswa kuwa kiongozi wa familia na kuwajali wote, mkewe akiwemo. Wimbo huu pia unadhihirisha unyanyasaji wa mwanamke, swala linaloendelezwa na wanaume.

Kwa jumla, wimbo huu unaonyesha mwelekeo wa kijamii wa kutothamini mwanamke akasahaulika kila wakati. Maudhui katika wimbo huu yamechanganuliwa katika misingi ya ufeministi wa Kiafrika, kwani huku kunyanyaswa kwa mwanamke katika misingi ya uana na utamaduni

kwapaswa kuondolewa kwa kusawazisha wanadamu wote kwa upande wa utamaduni na uana. Haya ni kwa mujibu wa mihimili ya nadharia hii.

Mwimbaji : Nguri
Umri: 76
Tarafa: Central
Lokesheni: Municipality
Kata : Iveche
Tarehe : 19/10/07

2.2.6 Muviki theka

Muviki theka x2
i-i-yia-i muviki theka, muviki theka-i-ai
Toria waathekire mukiendana
Ayia-i-i, muviki i theka ayia
Muviki theka ayia.
Mburi ciaukire ikithekaga
Ayia-i-i mburi ciaukire ikithekaga
Muviki theka x 2

I-i-yia-i muviki theka -ayia
Ng'ombe ciukire ikithekaga
Ayia-i-i ng'ombe ciaukire ikithekaga
Muviki theka x 2

Tafsiri kwa Kiswahili

Cheka Bi harusi

Cheka Bi-harusi x 2
Salaale! Cheka, cheka Bi harusi
Kama ulivyocheka mulipokutana na kupendana na Bwana harusi

Mbuzi tuliotoa kama mahari walicheka ajabu
Cheka Bi-harusi x 2
Salaale! Cheka, cheka Bi arusi

Ng'ombe tuliotoa kama mahari walicheka ajabu
Cheka Bi harusi x2
Salaale! Cheka, cheka Bi harusi
Bi harusi cheka x 2

Wimbo huu uliimbiwa Bi-harusi na watu wa upande wa Bwana harusi kusudi kumkaribisha katika makao yake mapya. Alishauriwa kucheka kama alivyocheke walipokutana mara ya kwanza na Bwana harusi. Aidha, Bi harusi alishauriwa kucheka kama mahari ya mbuzi, na ng'ombe ilivyocheke.

Maudhui yaliyopatikana katika wimbo huu ni furaha katika ndoa.

Bi harusi ashauriwa kucheka kama alivyocheke walipokutana na Bwana harusi.

Wimbo huu pia wabainisha thamani iliyopewa ndoa katika jamii ya Waembu. Ni dhairi kwamba ng'ombe na mbuzi walitolewa kama mahari. Mifugo hawa walithaminiwa sana katika jamii hii na waliweza kutolewa katika shughuli zilizothaminiwa sana katika jamii. Mfano wa shughuli kama hizi ni ndoa kuhusishwa kwa mke na mbuzi na ng'ombe pamoja na wazo kuwa mwanamke angeweza kubadilishwa na mahari ni maudhui yanayosusha heshima ya mwanamke katika jamii. Nadharia ya ufeministi wa Kiafrika imetumika kuchanganua maudhui katika wimbo huu, kwani mwanamke kuhusishwa na mbuzi na ng'ombe kwaeleza kwa uyakinifu hali inayomkumba mwanamke katika jamii ya Waembu. Nadharia ya uhalisia inaweza kutumika kuchanganua maudhui haya, kwani

imetufafanulia wazi uhalisi wa jamii ya Waembu ambapo mifugo ilithaminiwa sana.

Mwimbaji : Matenguri Mwita Njau
Umri: 90
Tarafa: Central
Lokesheni: Municipality
Kata : Kangaru
Tarehe : 19/10/07

2.2.7 Muviki Kavora

Muviki kavora x2
Niathinjirwe nguku x2
Muviki kavora x2
Niathinjirwe mburi x2
Muviki kavora x2
Niathinjirwe ng'ombe x2
Muviki kavora x2
Niakundwe iria

Tafsiri kwa Kiswahili

Bi Harusi pole pole

Bi harusi pole pole x2
Bi harusi achinjiwe kuku x2
Bi harusi pole pole x2
Bi harusi achinjiwe mbuzi x2
Bi harusi pole pole x2
Bi harusi achinjiwe ng'ombe x2
Bi harusi pole pole x2
Bi harusi apewe maziwa

Wimbo huu uliimbwa baada ya harusi miongoni mwa watu wa jamii ya jadi ya Waembu wakati wa kusindikiza Bi harusi hadi nyumbani mwake atakamoishi tangu siku hiyo. Kupitia wimbo huu, Bi harusi alishauriwa kuwa na subira maishani. Ujumbe huu ulipitishwa kupitia maneno yafuatayo – *muviki kavora* (Bi harusi pole pole). Aidha, ulitoa ujumbe

kwamba Bi harusi ni mtu aliyethamaniwa sana na jamii kwa jumla, ndiyo maana watu walikuwa tayari kumpa kuku, mbuzi, ng'ombe, maziwa n.k. Vitu ambavyo vilithamaniwa sana.

Wimbo huu ulishirikisha maudhui ya maadili mema maishani mwa Bi harusi, haswa alipoambiwa aende pole pole. Kwenda pole pole huku kuliashiria subira au kufikiria sana kabla ya kukata shauri kuhusiana na maswala ya kijamii kusudi kujenga jamii kielelezo. Uhalisia kama nadharia imetumika kuchanganua maudhui katika wimbo huu ambapo yadhihirisha uhalisi wa maisha ya wakati huo ambapo subira na maadili mema ni mambo yaliyothamaniwa sana katika jamii ya Waembu. Mtu yeyote aliyekuwa na subira aliheshimiwa sana katika jamii.

Mwimbaji : Mugo Nginyirwa
Umri: 76
Tarafa: Nembure
Lokesheni: Gatari South
Kata : Nembure
Tarehe : 20/10/07

2.3 HITIMISHO

Sura hii imebainisha nyimbo za harusi za jamii ya Waembu za kabla ya maingilio ya wakoloni. Tafsiri ya nyimbo hizi kwa Kiswahili imetolewa. Aidha maelezo na maudhui katika kila wimbo yametolewa. Maudhui ya jumla yaliyoshamiri katika nyimbo hizi yamebainika kama maadili mema katika jamii, ushirikiano baina ya mume na mke katika kujenga jamii mpya ya Waembu iliyokubalika kitamaduni, ubaguzi wa wanawake kijinsia, thamani kubwa iliyopewa asasi ya ndoa katika jamii ya Waembu kabla ya maingilio ya wakoloni na majigambo ya mwanamke kwa uwezo wake kuzaa mtoto msichana. Nadharia ya uhalisia na ya ufeministi wa Kiafrika imetumiwa kuchanganua maudhui haya, haswa kwa kuzingatia jinsi nyimbo hizi zilivyomsawiri mwanamke katika jamii pamoja na kuonyesha uhalisi wa kijamii katika jamii ya Waembu ya wakati huo.

Sura ya tatu inayofuata inashughulikia nyimbo za harusi za jamii ya Waembu za baada ya maingilio ya wakoloni pamoja na kuchanganua maudhui yaliyoshamiri katika nyimbo hizi.

SURA YA TATU

3.0 UTANGULIZI

Sura hii inashughulikia nyimbo za harusi za jamii ya Waembu za baada ya maingilio ya wakoloni pamoja na kuchanganua maudhui katika nyimbo hizi. Kwanza, nyimbo ziliandikwa kwa lugha ya Kiembu kisha kutafsiriwa kwa Kiswahili. Maudhui katika nyimbo nyingi za harusi miongoni mwa watu wa jamii ya Waembu yalionekana kubadilika. Kubadilika huku kuna misingi yake katika kauli ya King'ei na Kisovi (2005:7-8) kwamba wimbo ni utanzu wa fasihi simulizi ulio hai ambao hukua na kubadilika kutokana na mpito wa wakati na mabadiliko ya mfumo wa jamii. Mabadiliko haya hutokana na haja, wakati na mazingira. Mabadiliko ni lazima yawepo kulingana na maendeleo ya jamii. Kufuatia mabadiliko haya ya maudhui, nyimbo nyingi za harusi zilikuwa na maudhui ya dini ambapo uwezo wa Mungu ulitambuliwa, usawa wa kijinsia kati ya mke na mume, maudhui ya kuburudisha yalianza kushamiri katika nyimbo, thamani kubwa iliyopewa uchumi wa pesa ilitambulika, mapenzi yalizungumziwa katika nyimbo hadharani, aidha umuhimu wa kufanya ndoa takatifu kanisani ulisisitizwa. Hata hivyo, baadhi ya maudhui yaliendelea kutoka kipindi cha kabla ya maingilio ya wakoloni kwenda hadi kipindi cha baada ya maingilio ya wakoloni. Mfano wa maudhui kama haya ni maadili mema katika jamii, ushirika maishani, pamoja na umuhimu wa ndoa katika jamii. Ifuatayo ni

mifano ya nyimbo kuonyesha kwamba maudhui yalibadilika huku mengine yakiendelea.

3.1 Gwikirwa Mbete

*Riu nimwathii gwikirwa mbete
Niyo mukwa wa kumuovania
Na mukwa uyu ti wa kavinda
Wigage nginya ugakua*

*Turagai muri andu airi
Vatikagie wingi karigati
Kuri thina na kuri utonga
Gwi kieva kana gikeno*

*Kiria Ngai agwatanithitie
Mundu ndakakigwatanure
Kiria Ngai atuite kitheru
Mundu ndakakithukie*

*Ngai ariki wira wa kuumba
Erire Adamu na Ewa
"Ciaranai mwicure nthi yonthe"*

*Ciana ni ndathimi cia Ngai
Imenyagirirei
Irutei kumenya Ngai
Tonde ti cienyu ni ciake*

*Mwathani atakire nyomba
Amiaki ni wira wa mana
Mwigitie amwakire mucii*

Tafsiri ya Kiswahili

Kufunga Pete

Sasa mumeenda kufunga pete
Pete hii ni mkufu wa kuwafunga,
Si kufungwa kwa muda tu
Ni kufungwa milele hadi kufa

Muishi nyote wawili milele
Kusiwe na mwingine kati yenu
Kukiwa na umaskini au utajiri
Kukiwa na furaha au huzuni

Chochote Mungu alichoweka pamoja
Hakuna mwenye ruhusa kukitenganisha
Chochote kilichotakaswa na Mungu
Hakuna mwenye ruhusa kukichafua

Mungu alipomaliza kuumba Adamu na Hawa
Aliwaambia wazae hadi kujaza ulimwengu
Watoto ni baraka kutoka kwa Mungu
Watunzeni na muelewe kwamba watoto hawa ni wa Mungu si wenu
Kuwatunza watoto ni kufanya kazi ya Mungu

Hakikisheni kwamba mwamuweka Mungu mbele ya yote mnayofanya
Kwani Mungu ni mwenye uwezo mkuu.

Waimbaji: kwaya ya kanisa Karingari
Tarehe: 21/10/07

Wimbo huu uliimbwa na bado huimbwa wakati maharusi wanapokaribia kuvishana pete baada ya hatua zote za harusi kukamilika. Wimbo huu huwakumbusha maharusi kwamba ndoa yao yapaswa kudumu milele kama Mungu alivyoagiza, wapaswa kumtegemea Mungu katika mambo yote wafanyayo maishani, wapaswa kujua kwamba wana jukumu la kuzaa watoto kujaza dunia kama alivyoagiza Mungu. Mwisho, maharusi wakumbushwa kwamba wanalo jukumu la kuwatunza watoto watakojaliwa, kwani huwa si wao bali ni wana wa Mungu.

Maudhui ya uwezo mkubwa alionao Mungu ni bayana katika wimbo huu. Haya ni dhahiri kutokana na imani kubwa watu waliyo nayo kwa Mungu. Wao wasema kwamba Mungu tu ndiye mwenye uwezo wa kuwajalia watu kupata watoto wanaothaminiwa sana maishani pamoja na chochote

watakacho maishani, kwani wao wenyewe hawana uwezo wa kujitegemea bila Mungu kuwepo.

Aidha, wimbo huu unadhihirisha maudhui ya maadili mema yaliyojengeka katika misingi ya dini, wala si itikadi za kitamaduni. Haya ni bayana, haswa tukizingatia vifungu vifuatavyo katika wimbo huu:-

**Sasa mumeenda kufunga pete,
Huu ni mkufu wa kuwafunga
Milele kama aagizavyo Mungu.....**

Kifungu hiki chatoa onyo kwamba ni kinyume na maadili ya dini kutalikiana baada ya wawili kufunga ndoa.

**Watoto ni baraka kutoka kwa Mungu, mkijaliwa kuwapata,
wafunzeni maadili mema kama alivyoagiza Mungu huku mkielewa
fika kwamba wana hawa si wenu bali ni wa Mungu....**

Kifungu hiki pia chasisitiza maudhui ya maadili mema yaliyojengeka katika misingi ya dini.

3.2 Uviki Mutheru

*Nimweka uviki mutheru x 2
Andu a kanitha ni aira
Mwanake ni watwika muthuri
Nduri mwanake ringi*

*Mwiritu ni watwika mutumia
Nduri mwiritu ringi*

*Mundu etagwa muthuri
Nikuthuthuria maundu na gutungata muka,
Etagwa mutumia, nigutumiria maundu na gutungata murume*

Tafsiri kwa Kiswahili

Ndoa Takatifu

Mumefanya ndoa takatifu x 2

Waumini wote wa kanisa ni mashahidi.

Mume huitwa mume kwa kuitunza jamii yake na kuwa na subira maishani

Mke huitwa mke kwa kunyenyekea kwa mume wake kila wakati

Mume huitwa mume kwa kumnyenyekea mke wake

Waimbaji: kwaya ya kanisa Karingari

Tarehe: 21/10/07

Wimbo huu huimbwa katika harusi ya jamii ya Waembu baada ya maharusi kuvishana pete. Jukumu la wimbo huu ni kuwatahadharisha wafungao ndoa kwamba maisha baada ya ndoa yafaa kuchukuliwa kwa uzito zaidi kinyume na maisha ya hapo awali katika uvulana na usichana. Aidha, wimbo huu wadokeza kwamba mume apaswa kumpenda bibi yake, awe na subira kwake kwani yeye ni kiumbe dhaifu. Mke naye ashauriwa kumtii mume wake kwani yeye ndiye kiongozi wa familia.

Maudhui ya usawa wa majukumu ya kijamii kati ya mume na mke yanadhihirika katika wimbo huu. Mwanamke ameshauriwa kuwa mnyenyekevu kwa mume wake huku mumewake naye akishauriwa kunyenyekea kwake pia.

Tazama yafuatayo:-

... mke huitwa mke kwa kunyenyekea kwa mumewe kila wakati, mume naye huitwa mume kwa kuwa na subira na kunyenyekea mkewe

Maudhui ya maadili mema katika ndoa yenye misingi ya kidini yanadhihirika katika wimbo huu. Haya ni kutokana na kuingia katika maisha takatifu ya ndoa. Maharusi wapaswa kufuata maadili mema kulingana na mafunzo ya dini.

3.3. Kimuri

Giki nikio kimuri
Giki-i nikio kimuri
Kimurikitwe ni Ngai
Ayia – ui – kimuri x2

Giki-i nikio kimuri
Kimurikitwe ni ciana
Ayia – ui – kimuri x2

Giki-i nikio kimuri
Kimurikitwe ni aciari
Ayia – ui- kumuri x2

Giki-i nikio kimuri
Kimurikitwe ni rwendo
Ayia –i –ui- kimuri x2

Tafsiri kwa Kiswahili

Mwangaza

Huu ndio mwangaza
Ulioangaziwa na Mungu
Huu ndio mwangaza x2

Huu ndio mwangaza
Ulionangaziwa na watoto wetu
Huu ndio mwangaza x 2

Huu ndio mwangaza
Ulionangaziwa na wazazi
Huu ndio mwangaza x2

Huu ndio mwangaza
Ulioangaziwa na mapenzi
Huu ndio mwangaza x2

Waimbaji: kikundi cha akina mama cha *Murugi*
Tarehe: 22/10/07

Wimbo huu huimbwa baada ya Bwana na Bi harusi kuvishana pete. Ujumbe kwenye wimbo huu ni kwamba harusi takatifu ni mwangaza maishani. Mwangaza huu huletwa na Mungu, mapenzi, wazazi pamoja na maharusi wenyewe. Wimbo huu unaangazia furaha inayoweza kupatikana katika ndoa iliyotawaliwa na Mungu, mapenzi na ushauri wa wazazi wa maharusi.

Wimbo huu waeleza bayana kwamba harusi takatifu ina dhima kuu katika jamii, kwani huwa ni mwangaza maishani. Mwangaza huu husaidia kujenga jamii kielelezo. Hebu tazama kifungu kifuatacho cha wimbo huu:

Giki-i nikio kimuri.... (hii harusi ni mwangaza.....).

Malezi bora ya watoto yenye misingi yake katika maadili ya dini ni maudhui bayana katika wimbo huu. Maudhui haya yanabainika katika wimbo huu ambapo wimbo unaeleza kwamba wazazi wanalo jukumu la kuwaongoza watoto wao hadi kuwa watu wazima watakaobiletea jamii mwangaza, haswa tukirejelea kifungu kifuatacho katika wimbo huu:

Giki-i nikio kimuri
Kimurikitwe ni aciari
Ayia – ui – kimuri x2

Tafsiri
Huu ndio mwangaza
Ulioangaziwa na wazazi
Huu ndio mwangaza x2

Mwangaza ulioangaziwa na wazazi kwa maharusi unaozungumziwa hapa ni malezi bora yenye kufuata maadili ya kidini kutoka utotoni hadi uzimani na wakati wa kufunga ndoa.

Maudhui ya mapenzi pia ni bayana katika wimbo huu. Haya ni bayana haswa tukirejelea kifungu kifuatacho kutokana na wimbo huu:

Giki-i nikio kimuri
Kimurikitwe ni rwendo
Ayia –i – ui – kimuri x2

Tafsiri
Huu ni mwangaza
Ulioangaziwa na mapenzi
Huu ndio mwangaza x2

Mapenzi kati ya Bwana na Bi harusi yanazungumziwa hapa pamoja na umuhimu wa kuyadumisha kwani hulete furaha na mwelekeo katika jamii.

3.4 *Nimburia Nindungwe*

Nimburia ni ndungwe x2
Wanangatungwa na mburi
Kana ngatungwa na njau
Icio cionthe ndingyoca
Mumenye mwana ari 'vinya
Agikaathii na maguru agikoneka

Nimburia ni ndungwe x2
Wanangatungwa na uki
Kana ngatungwa na iria
Icio cionthe ndingyoca
Mumenye mwana arivinya
Agikaathii na maguru agikoneka

Tafsiri kwa Kiswahili

Nikaribishwe

Nikaribishwa x2
Hata nikikaribishwa kwa kupewa mbuzi
Au nikaribishwa kwa kupewa ndama
Siwezi nikakubali
Mwapasa kufahamu kwamba ni vigumu
Sana kumlea mwana pamoja na kumzaa.

Nikaribishwe x2
Hata nikikaribishwa kwa kupewa asali,
Au nikaribishwe kwa kupewa maziwa,
Siwezi nikakubali,
Mwapasa kufahamu kwamba ni vigumu
Sana kumlea mwana pamoja na kumzaa

Nikaribishwe x2
Hata nikikaribishwa kwa kupewa asali,
Au nikaribishwe kwa kupewa maziwa,
Siwezi nikakubali,
Mwapasa kufahamu kwamba ni vigumu
Sana kumlea mwana pamoja na kumzaa

Waimbaji: Kikundi cha akina mama cha *Murugi*
Tarehe: 22/10/07

Wimbo huu huimbwa wakati wazazi wa Bi. Harusi wanapoingia katika boma ya Bwana harusi baada ya kufunga ndoa. Ujumbe unaopatikana

katika wimbo huu ni kwamba wazazi wa Bi harusi na washirika wao waona fahari kubwa ya kuwa na msichana aliyeolewa ambaye thamani yake ni kubwa kuliko kitu kingine chochote katika jamii kama maziwa, asali, ng'ombe na mbuzi.

Wimbo huu una maudhui ya ukarimu. Haya ni dhahiri kutokana na kule kuomba kwa wazazi wa Bi harusi kukaribishwa pale nyumbani kwa Bwana harusi.

Tazama

Nimburia ni ndungwe x2 (Naomba kukaribishwa)

Wimbo huu huimbwa kuwakumbusha Bi na Bwana harusi kuwa wapaswa kuwa watu wakarimu katika maisha yao ya baadaye.

Aidha wimbo huu una maudhui yanayobainisha jinsi mwana anavyoonewa fahari katika jamii ya Waembu. Haya yanabainika, haswa tukirejelea kifungu kifuatacho cha wimbo huu:

Mumenye mwana arivinya agikaathii na maguru agikoneka x2

Tafsiri

Mfahamu kwamba ni vigumu kumpata mtoto, kumtunza hadi kufika wakati wa kuwa mtu mzima wa kuo au kuolewa. Huu ni ushauri kwa maharusi kuwatunza watoto iwapo watajaliwa

Maudhui mengine yanayopatikana katika wimbo huu ni thamani ya mali katika maisha ya ndoa. Wimbo huu wadokeza kwamba mali kama vile mifugo (ng'ombe, mbuzi n.k) huwa ni muhimu katika maisha ya ndoa na maharusi wapaswa kuitafuta na kuitunza iwapo watafanikiwa kuipata. Hii ni kwa sababu mali hutumiwa kulipa mahari pamoja na kuwakaribisha wazazi wa Bi harusi nyumbani kwa Bwana harusi. Kwa kuwa wazazi wa msichana hukubali kubadilisha mali kwa msichana wao wanayemthamini zaidi, basi mali huwa ni muhimu maishani.

3.5 Muviki

Mukui: Muviki-i kuthakara x3
Onthe: Muviki-i kuthakara x3

Mukui: Muviki-i ni maua x3
Onthe: Muviki-i ni maua x3

Mukui: Muviki-i ni gikeno x3
Onthe: Muviki-i ni gikeno x3

Mukui: Muviki-i kurungara x3
Onthe: Muviki-i kurungara x3

Mukui: Muviki-i kuririmba x3
Onthe: Muviki-i kuririmba x3

Tafsiri kwa Kiswahili

Bi harusi

Kiongozi: Bi harusi mrembo x3
Wote: Bi harusi mrembo x3

Kiongozi: Bi harusi ni maua x3
Wote: Bi harusi ni maua x3

Kiongozi: Bi harusi ni furaha x3
Wote: Bi harusi ni furaha x3

Kiongozi: Bi harusi amenyooka x3
Wote: Bi harusi amenyooka x3

Kiongozi: Bi harusi anametameta x3
Wote: Bi harusi anametameta x3

Waimbaji: Kikundi cha akina mama cha *Murugi*
Tarehe: 22/10/07

Wimbo huu huimbwa na watoto katika sherehe ya harusi miongoni mwa watu wa jamii ya Waembu wakati watu wametulia kula chakula kilichoandaliwa.

Maudhui katika wimbo huu huwa ni sifa kwa Bi harusi kusudi kumuonyesha vile anavyopewa heshima na wote. Pamoja na hayo, wimbo huu hutekeleza jukumu la kuburudisha watu haswa ikizingatiwa kuwa huimbwa na watoto ambao hawawezi kupewa jukumu la kupitisha ujumbe wowote muhimu miongoni mwa watu wa jamii ya Waembu.

3.6 Nthumbi

Mukui: Nthumbi ya mwana kuthakara ithatitwe na maua ma mbesa –i

Onthe: Nthumbi ya mwana kuthakara ithatitwe na maua ma mbesa-i

Mukui: Nthumbi ya mwana

Etikia: Kuthakara

Mukui: Ithatitwe na.....

Etikia: Maua ma mbesa –i

Mukui: Neti ya mwana kuthakara ithatitwe na maua ma mbesa-i

Onthe: Neti ya mwana kuthakara ithatitwe na maua ma mbesa-i

Mukui: Neti ya mwana

Etikia: Kuthakara

Mukui: Ithatitwe na...

Etikia: Maua ma mbesa-i

Mukui: Nyomba ya mwana kuthakara ithatitwe na maua ma mbesa-i

Onthe: Nyomba ya mwana kuthakara ithatitwe na maua ma mbesa-i

Mukui: Nyomba ya mwan

Etikia: kuthakara

Mukui: Ithatitwe na.....

Etikia: Maua ma mbesa-i

Tafsiri kwa Kiswahili

Taji

Kiongozi: Taji la Bi harusi maridadi limerembeshwa kwa maua ya pesa

Wote: Taji la Bi harusi maridadi limerembeshwa kwa maua ya pesa

Kiongozi: Taji la Bi harusi....

Wote: Kurembeka

Kiongozi: Limerembeshwa kwa....

Wote: Maua ya pesa-i

Kiongozi: Neti ya Bi harusi maridadi imerembeshwa kwa maua ya pesa

Wote: Neti ya Bi harusi maridadi imerembeshwa kwa maua ya pesa-i

Kiongozi: Neti ya Bi harusi...

Wote: Maridadi

Kiongozi: Imerembeshwa kwa

Wote: Maua ya pesa-i

Kiongozi: Nyumba ya Bi harusi maridadi imerembeshwa kwa maua ya pesa-i

Wote: Nyumba ya Bi harusi maridadi imerembeshwa kwa maua ya pesa-i

Kiongozi: Nyumba ya Bi harusi.....

Wote: Maridadi

Kiongozi: Imerembeshwa kwa....

Wote: maua ya pesa-i

Waimbaji: Kikundhi cha akina mama cha *Murugi*

Tarehe: 23/10/07

Wimbo huu huimbwa wakati wa kutoa zawadi kwa maharusi miongoni mwa watu wa jamii ya Waembu. Wimbo huu hujenga taaswira ya urembo na mapambo ya Bi harusi na kufananisha kujipamba huku na urembo wake na ule wa pesa.

Wimbo huu unasheheni maudhui ya thamani kubwa inayopewa uchumi wa pesa katika jamii. Haya yaeleweka waziwazi kutokana na usemi kwamba nyumba ya Bi harusi, taji lake, pamoja na neti yake vyote vimerembeka kwa kuwa vimerembeshwa kwa kuwekwa maua ya pesa.

3.7 *Twauka maguru*

Onthe: Twauka maguru-u kanyanya wetu ii ayia, twauka maguru ni undu wa gukwenda

Mukui: Kanyanya wa mwana-i

Etikia: Twauka maguru

Mukui: Muvikania wetu-i

Etikia: Twauka maguru

Mukui: Na muviki wetu-i

Etikia: Twauka maguru

Mukui: Twonthe twonthe twonthe

Etikia: Twauka maguru

Tafsiri kwa Kiswahili

Tumetembea

Wote: Tumetembea kuja hapa wazazi wa mume wa binti yangu. Tumekuja kwa miguu kwa sababu ya kuwapenda.

Kiongozi: Wazazi wa Bwana harusi-i tumetembea kuja hapa kwa sababu ya kuwapenda.

Wote: Tumetembea kuja hapa

Kiongozi: Bwana arusi

Wote: Tumetembea kuja hapa

Kiongozi: Bi harusi wetu

Wote: Tumetembea kuja hapa

Kiongozi: Sote! Sote! Sote!

Wote: Tumetembea kuja hapa

Waimbaji: Kikundi cha akina mama cha *Murugi*

Tarehe: 24/10/07

Wimbo huu huimbwa katika harusi za Kiembu wakati watu wa familia ya Bi harusi wanaingia kwenye boma ya Bwana harusi baada ya kufunga pete. Kupitia wimbo huu, wao husema kwamba wametembea kwa miguu kuhudhuria ile harusi kwa mapenzi waliyonayo kwa Bwana harusi, Bibi harusi na familia ya Bwana harusi kwa jumla.

Waimbaji wasema kuwa mapenzi waliyonayo kwa Bwana na Bibi harusi yamewafanya wakatembea kuhudhuria ile harusi. Ujumbe wa wimbo huu

huwa umekusudiwa kupita kwa maharusi hivi kwamba wataweza kudumisha mapenzi katika ndoa yao kwani mapenzi ni muhimili muhimu katika ujenzi wa jamii kupitia ndoa.

Aidha, maudhui ya kujitolea kufanya kazi kwa bidii yanajitokeza kupitia wimbo huu haswa tukirejelea ukweli kwamba wazazi wa Bi harusi na wengine walitembea kwa miguu kuhudhuria harusi hiyo. Walivumilia ule uchovu wote. Ujumbe huu huwa ni ushauri kwa maharusi kuwa na bidii ili kufaulu maishani.

3.8 Niakindwe suka

Mukui: Niakindwe i-i niakindwe suka x2

Etikia: Akirugira ciana akoragwe ari muthaka x2

Mukui: Niekire -i-i niekiwe nthumbi x2

Etikia: Akirugira ciana akoragwe ari muthaka x2

Tafsiri kwa Kiswahili

Afungwe Kanga

Kiongozi: Afungwe! Afungwe! Shuka x2

Wote: Akiwapikia watoto wake awe nadhifu

Kiongozi: Avalishwe! Avalishwe taji x2

Wote: Akipikia watoto awe nadhifu x2

Uliimbwa katika harusi ya Sally Munyi na Carol Murugi
Tarehe: 24/11/07

Wimbo huu huimbwa katika sherehe ya harusi ya Kiambu wakati wa kumtakaza Bibi harusi na kumfanya kuwa mke halisi kwa kumfunga

kanga kiunoni mwake kama atakavyojifunga akitekeleza shughuli zake za kila siku pale nyumbani. Wimbo huu humkumbusha wajibu anaopaswa kutekeleza kama mwanamke wa kuwatunza watoto pamoja na Bwanake.

Wajibu wa mwanamke nyumbani unabainika kupitia wimbo huu ambao ni kuwatunza watoto na mumewe, haswa kwa kuwapikia na kuwalisha vizuri. Aidha unadhifu wa mwanamke ni swala linalotiliwa maanani. Unadhifu unaozungumziwa hapa ni wa mavazi na tabia za mwanamke baada ya kuolewa.

3.9 Ngatho

Nitwacokia ngathox2

Kwa murata wetu

Ngai arogutethia uciare muthamaki

Murithie cionthe-i

Wana njau x2

Cionthe cionthe -i

Wana njau

Tafsiri kwa Kiswahili

Tumeshukuru

Tumeshukuru x2

Tumeshukuru rafiki wetu

Mungu akubariki uwe mama wa mfalme

Akubariki uweze kupata ng'ombe wengi

Uwafuge wote!

Wote! Wote! Wote!

Pamoja na ndama!

Ndama wengi zaidi

Huu ni wimbo wa shukurani. Huimbwa na wote katika harusi ya Kiambu kuonyesha shukurani za waliohudhuria harusi kwa ukarimu wa Bi harusi. Watu humwombea Bi harusi baraka kutoka kwa Mungu. Haswa yeye huombewa kupata mwana wa kiume atakayekuwa mfalme. Aidha Bi harusi huombewa baraka za Mungu kupata mifugo tele.

Wimbo huu unamaudhui ya uungu ambapo uwezo wa Mungu wa kubariki maharusi katika ndoa unazungumziwa. Haya ni kutokana na kidokezo kwamba Mungu ana uwezo wa kubariki maharusi kupata mwana na kumtunza mwana huyu hadi kuwa mfalme. Aidha, uungu unapatikana tukirejelea ujumbe katika wimbo huu kwamba Mungu anaweza kuwabariki maharusi kupata mifugo pamoja na mali nyingi kusudi kuwawezesha kuwa na raha maishani

Thamani ya mali ni maudhui mengine yanayojitokeza katika wimbo huu. Haya yanathibitishwa na ombi litolewalo katika wimbo huu kwamba Mungu awabariki maharusi kupata mali ya kila aina.

Maudhui mengine yanayojitokeza katika wimbo huu ni utukufu na heshima inayopewa wenye mamlaka ya kuiongoza jamii. Haya ni kutokana na ombi kwamba maharusi wabarikiwe kupata mwana atakyekuwa mfalme katika jamii.

Uliimbwa katika harusi ya Justa Muthoni na Kinyua Nthambiri iliyofanyika katika kijiji cha Rung'ang'a wilayani Embu tarehe 24/11/2007.

3.10 Athamaga na Ng'ombe

*Muvikania wetu ii
Athamaga na ng'ombe
Ukai mwone x2
Muvikania wetu -i- uria agucaina*

*Muviki wetu ii
Athamaga na ng'ombe
Athamaga na mwitha
Ukai mwone x2 muviki wetu-i-
Uria agucaina*

Tafsiri kwa Kiswahili

Yeye huhama pamoja na ng'ombe wake
Bwana harusi
Huhama pamoja na ng'ombe njoo muone x2
Vile Bwana harusi anavyometameta

Bi harusi
Huhama pamoja na ng'ombe
Huhama pamoja na maziwa
Njoo muone x2
Jinsi Bi harusi anavyometameta

Wimbo huu una maudhui ya maadili mema katika jamii ambapo watu katika jamii wapaswa kutunza mali yao na chochote wajaliwacho. Haya

ni dhahiri kufuatia ujumbe kwamba Bi harusi huhama na ng'ombe, maziwa na chochote kilicho chake, ndiyo maana yeye huweza kuwa na furaha maishani.

Aidha, maudhui ya thamani kubwa inayopewa utajiri wa mifugo haswa ng'ombe, mbuzi, kondoo n.k ni dhahiri katika wimbo huu. Haya ni kutokana na ujumbe kwamba Bibi na Bwana harusi huhama pamoja na mifugo wao popote waendapo ili kuitunza. Utunzaji huu unaashiria thamani kubwa ya utajiri huu.

Uliimbwa katika harusi ya Sally Munyi na Carol Murugi – Nembure, Tarehe 24/11/07.

Kwa kifupi, maudhui yaliyoshamiri katika nyimbo za harusi za jamii ya Waembu za kipindi cha baada ya ukoloni ni uwezo na nguvu za Mungu, maadili mema yaliyojengeka katika misingi ya dini, usawa wa kijinsia (kati ya mume na mke), mapenzi, dhima ya mwana katika jamii, thamani ya uchumi wa pesa katika jamii, ukarimu, burudani na bidii kazini.

Haya yalikuwa mabadiliko ya maudhui yaliyotokea kiwakati katika nyimbo za harusi za Waembu. Mabadiliko haya yaweza kuelezwa katika misingi ya nadharia ya uhalisia wa kijamaa ambayo kwa mujibu wa Qusby (1988) na Larkin (1972) hulenga kuusawiri ulimwengu kama ulivyo. Kutokana na mpito wa wakati, mambo kadha wa kadha katika

jamii ya Waembu yamebadilika kudhihirisha uhalisi wa historia ya wakati wake. Katika misingi hii, maudhui ya nyimbo za harusi za jamii ya Waembu nayo yalibadilika sambamba na mabadiliko ya kijamii kutoka kipindi cha kabla ya maingilio ya wakoloni hadi baada ya maingilio hayo. Maudhui yaliyodhihirisha mabadiliko ya majukumu ya kiuana ya mwanamke yaweza kuelezwa katika misingi ya nadharia ya ufeministi wa Kiafrika ambapo wanawake walitaka kujitambulisha na kukoma kuwategemea wanaume. Hii ndiyo sababu baadhi ya nyimbo zilibeba maudhui yaliyoonyesha usawa wa majukumu ya kijamii kati ya mke na mume. Haya yalikuwa kinyume na wakati kabla ya maingilio ya wakoloni ambapo mwanamke alibaguliwa na kutengewa majukumu anuwai kijinsia.

3.2 HITIMISHO

Sura ya tatu imeshughulikia nyimbo za harusi za jamii ya Waembu za baada ya maingilio ya wakoloni. Nyimbo kumi za kipindi hiki zimeorodheshwa kwa lugha ya Kiembu, kutafsiriwa kwa Kiswahili pamoja na kujadili maudhui anuwai katika kila wimbo. Mwisho, imefafanuliwa kwamba maudhui haya yamebadilika kutoka yalivyokuwa katika nyimbo za harusi za jamii ya Waembu za kabla ya maingilio ya wakoloni. Mabadiliko haya yameelezwa kinadharia katika misingi ya uhalisia na ufeministi wa Kiafrika.

Sura ya nne inayofuata inashughulikia ulinganishaji wa maudhui katika nyimbo za harusi za jamii ya Waembu kabla na baada ya maingilio ya wakoloni kusudi kubainisha jinsi maudhui haya yalivyobadilika na kuendelea kutoka kipindi cha kabla ya maingilio ya wakoloni na baada ya maingilio hayo katika jamii ya Waembu.

SURA YA NNE

4.0 UTANGULIZI

Sura hii inashughulikia ulinganishaji wa maudhui ya nyimbo za harusi za jamii ya Waembu za kabla ya maingilio ya wakoloni na yale ya baada ya maingilio ya wakoloni. Lengo lilikuwa kubainisha jinsi maudhui yalivyobadilika kiwakati kuambatana na mabadiliko ya kihistoria katika jamii kama wanavyofafanua Nandwa na Bukenya (1983) kuwa kazi ya fasihi haitokei katika ombwe tupu, bali huchota maudhui yake katika jamii. Mabadiliko yatokeayo katika jamii kihistoria huenda sambamba na mabadiliko ya maudhui katika kazi ya fasihi, haswa fasihi simulizi.

Aidha sura hii inalenga kuonyesha maudhui yaliyoendelea kutoka kipindi cha kabla ya maingilio ya wakoloni hadi baada ya maingilio hayo. Yafuatayo ni maudhui yaliyobainika katika nyimbo za harusi miongoni mwa watu wa jamii ya Waembu.

4.1 MAUDHUI KATIKA NYIMBO ZA HARUSI ZA JAMII YA WAEMBU KABLA YA MAINGILIO YA WAKOLONI

Maadili mema katika jamii ni maudhui yaliyobainika waziwazi katika nyimbo za harusi za wakati huo. Maadili hayo yalikuwa na misingi yake

katika mila na itikadi za jamii ya Waembu zilizothaminiwa sana wakati huo. Baadhi ya mila hizi ni mke kunyenyekea mumewe, pamoja na wazazi wa mumewe, mume kuwaheshimu wazazi wa bibiye, mke kudumisha heshima yake baada ya kuolewa kwa kutoshirikiana na wasichana ambao hawajaolewa, n.k.

Ushirikiano wa mke na mume katika kujenga jamii kielelezo ni maudhui mengine yaliyopatikana katika nyimbo za harusi za jamii ya Waembu zilizoimbwa kipindi hiki. Ushirikiano huu ulionekana kama kiungo maalum cha kuiwezesha jamii kutafuta mali kusudi kuikimu familia pamoja na kuendeleza kizazi na jamii kwa jumla.

Ubaguzi wa mwanamke kijinsia ulibainika kama maudhui katika nyimbo za harusi za jamii ya Waembu za kipindi hiki. Mwanamke alionekana kama kiumbe dhaifu ambaye hapaswi kuwa na haki sawa na mwanamume, haswa tukirejelea kula chakula bora, kuishauri jamii kuhusu maswala muhimu, kufanya uamuzi kuhusu jambo lolote linalohusu maendeleo ya jamii, n.k.

Majigambo ya mwanamke nayo yalidhihirika katika nyimbo hizi. Sababu kuu ya majigambo hayo ilibainika kuwa uwezo wake wa kutunga mimba na kuzaa haswa mtoto msichana ambaye aliiwezesha jamii kuwa na

sherehe muhimu kama ya harusi. Aidha, mwanamke alijigamba kwa kuwa alijiona mwenye nafasi kubwa katika kuiendeleza jamii kupitia uzazi hata kuliko mwanamume.

Nyimbo za harusi za wakati huo pia zililenga kuonyesha dhima ya ndoa katika maudhui yake. Kupitia nyimbo hizi dhima hii ilidhihirika kama kuendeleza kizazi na jamii kwa jumla kupitia watoto waliopatikana katika ndoa. Dhima hii ilidhihirika kufuatia vitu vilivyotolewa kama mahari ambavyo vilithaminiwa sana kijamii, mifano ikiwa ni ng'ombe, mbuzi, pombe, asali na maziwa.

4.2 MAUDHUI KATIKA NYIMBO ZA JAMII YA WAEMBU ZA BAADA YA MAINGILIO YA WAKOLONI

Nyimbo zilizoimbwa kipindi hiki zilionyesha uwezo na nguvu za Mungu dhidi ya binadamu. Nguvu hizi zilikuwa uwezo wa kuunganisha Bibi na Bwana harusi daima baada ya kufunga ndoa. Aidha, uwezo huu unadhihirika katika nyimbo za kipindi hiki, haswa zinapobainisha kwamba Mungu aliwapa mke na mume uwezo wa kumsaidia kuumba binadamu kupitia uzazi. Hii ndiyo sababu baadhi ya nyimbo za kipindi

hiki zinabaini kwamba kuwalea watoto ni kufanya kazi kwa niaba ya Mungu.

Maadili mema katika jamii ni maudhui bayana katika nyimbo za kipindi hiki. Hata hivyo, nyimbo za kipindi hiki zilionyesha maadili mema katika jamii yaliyojengeka katika misingi ya dini, kinyume na ilivyokuwa kipindi cha kabla ya ukoloni ambapo maadili haya yalijengeka katika misingi ya mila na itikadi za jamii ya Waembu.

Usawa wa majukumu ya kijinsia kati ya mume na mke ni maudhui yaliyobainika katika nyimbo za kipindi hiki. Nyimbo nyingi za wakati huu ziliweka wazi kwamba mume apaswa kumheshimu mke na kutambua nafasi yake katika ujenzi wa jamii. Kwa upande mwingine, mke naye apaswa kumheshimu mumewe na kumtambua kama mshirika wake katika ujenzi wa familia na jamii pana kwa jumla.

Mapenzi kati ya mume na mke sasa yalianza kuzungumziwa kadamnasi kinyume na ilivyokuwa kipindi cha kabla ya maingilio ya wakoloni ambapo hayakuzungumziwa waziwazi. Kufuatia haya, mapenzi baina ya mke na mume ni maudhui ambayo yalishamiri katika nyimbo za jamii ya Waembu za baada ya maingilio ya wakoloni.

Dhima kuu ya ndoa katika jamii ilibainika kama maudhui ambapo shughuli hii iliheshimiwa sana, haswa kwa kuwa ilipelekea kupata watoto waliothaminiwa sana kijamii.

Thamani ya uchumi wa pesa katika jamii nayo ilidhihirika kama maudhui katika nyimbo za kipindi hiki. Nyimbo nyingi zilitukuza wajibu utekelezwao na pesa. Hata wakati mwingine kufananisha urembo wa Bi harusi na ule wa pesa katika nyimbo za harusi zilizoimbwa.

Mwisho, baadhi ya nyimbo zilibadilika kimtindo ambapo lengo lake lilikuwa kuburudisha tu.

4.3 MABADILIKO YA MAUDHUI KUTOKA KIPINDI CHA MAINGILIO YA WAKOLONI HADI KIPINDI CHA BAADA YA MAINGILIO YA WAKOLONI

Baada ya kulinganisha na kulinganua maudhui ya nyimbo za harusi za jamii ya Waembu, maudhui yalionekana kubadilika. Ifuatayo ni ithibati kwamba maudhui yalibadilika:

Maudhui ya maadili mema yalipatikana katika nyimbo za harusi za vipindi viwili vilivyoshughulikiwa. Maadili haya yalitawaliwa na itikadi

na mila za jamii ya Waembu katika nyimbo zilizoimbwa kabla ya maingilio ya wakoloni. Watu waliaminika kufuata maadili mema iwapo wangezingatia maadili mema kwa mujibu wa itikadi za jamii kama ukarimu, unyenyekevu wa mke kwa mumewe, heshima kwa wakubwa, haswa wazazi, bidii kazini n.k. kwa upande mwingine, watu waliaminika kutofuata maadili mema kwa kutenda mambo yaliyopigwa marufuku kama kukosa heshima, ulafi, uzembe, kukosa ukarimu n.k. Baada ya maingilio ya wakoloni, maudhui ya maadili mema katika nyimbo za harusi za jamii ya Waembu yalibadilika ambapo kigezo cha kupimia utenda wema au ubaya wa mtu kilikuwa ni Biblia au mafunzo ya dini, bali si mila na itikadi kama ilivyokuwa hapo awali kabla ya maingilio ya wakoloni. Maudhui ya maadili mema yalisawiriwa tofauti katika vipindi hivi viwili kufuatia misingi tofauti ya kupimia maadili haya iliyojadiliwa hapa juu. Kuoja wake, wengi kwa mfano, ni kinyume na maadili mema katika misingi ya dini, bali ilikubalika katika mila na itikadi za jamii ya Waembu.

Maudhui ya ubaguzi wa mwanamke kijinsia yaliyopatikana katika nyimbo za kabla ya maingilio ya wakoloni yalibadilika na kusawiri usawa wa kijinsia kati ya mke na mume katika nyimbo za harusi zilizoimbwa baada ya maingilio ya wakoloni. Mke na mume walichukuliwa kuwa na nafasi sawa katika ujenzi wa jamii. Hii ni kufuatia kubadilika kwa

mwelekeo wa kijamii kuhusu nafasi ya mwanamke uliochangiwa na mapisi. Mwelekeo huu ulibadilika kutoka hasi kwenda chanya ambapo mwanamke alianza kuthaminiwa.

Maudhui ya Uungu (uwezo wa Mungu), pamoja na nafasi yake katika nyimbo zilizoimbwa katika harusi ya jamii ya Waembu baada ya maingilio ya wakoloni yalikuwa dhahiri. Maudhui haya yalichukua nafasi ya uume (uwezo mkubwa wa mwanamume) uliotukuzwa katika nyimbo nyingi zilizoimbwa katika harusi za Kiembu za kabla ya maingilio ya wakoloni, huku mwanamke akionywa iwapo hangenyenyekea kwa mumewe. Mabadiliko yaliyotokea ni kwamba mke na mume walipaswa kumnyenyekea Mungu wala si chochote au yeyote kama ilivyokuwa hapo awali kwa mujibu wa itikadi za kijamii. Hii ndiyo sababu iliyochangia kuwepo kwa nyimbo nyingi zenye maudhui ya Uungu baada ya maingilio ya wakoloni.

Baada ya maingilio ya wakoloni, nyimbo za harusi zilisheheni maudhui yaliyothamini uchumi wa pesa. Haya yalikuwa ni mabadiliko kutoka kipindi cha kabla ya maingilio ya wakoloni ambapo uchumi uliothaminiwa ni wa mifugo kama ng'ombe, mbuzi, kondoo, punda na mazao ya aina mbalimbali kutoka shambani. Hapo awali, nyimbo zilisheheni ujumbe kwamba maisha baada ya harusi yangekuwa na raha

iwapo maharusi wangepanya bidii kupata mifugo na mavuno mengi kutoka shambani. Baada ya maingilio ya wakoloni uchumi wa pesa ulitukuzwa na kuaminika kuchukua nafasi kubwa katika kulete furaha maishani. Hii ndiyo sababu nyimbo nyingi zikasheheni maudhui kama hayo.

Majigambo ya mwanamke yalitoweka kabisa kama maudhui katika nyimbo za harusi za jamii ya Waembu baada ya maingilio ya wakoloni. Haya ni kufuatia ufunuo kwa mwanamke kwamba uwezo wa kujifungua au kupata mtoto iliyokuwa sababu ya majigambo yake ulikuwa mikononi mwa Mungu. Hii ndiyo sababu iliyochangia wanawake kuimba nyimbo za kumtukuza Mungu katika harusi za Kiembu baada ya maingilio ya wakoloni.

Baada ya maingilio ya wakoloni maudhui ya mapenzi yalibadilika kimtindo ambapo nyimbo za kipindi hiki zilianza kuwa na mtindo uliozungumzia mapenzi kati ya mume na mke kadamnasi. Mtindo huu ni kinyume na wa kabla ya maingilio ya wakoloni ambapo mtindo katika nyimbo za wakati huo zilizungumzia mapenzi kati ya mke na mume kwa mafumbo, kwani kuyazungumzia hadharani ni swala lililopigwa marufuku katika jamii. Sababu hii ilichangia kuwepo na nyimbo nyingi

sana zilizoshughulikia mapenzi kwa kina katika harusi za jamii ya Waembu za baada ya maingilio ya wakoloni.

Ingawa maudhui katika nyimbo za harusi za jamii ya Waembu yalibadilika, kuna maudhui ambayo yalionekana kuendelea kutoka kipindi cha kabla ya maingilio ya wakoloni kwenda kile cha baada ya maingilio hayo. Mfano wa maudhui kama hayo ni yale yaliyozungumzia ushirikiano wa mke na mume katika kujenga jamii kielelezo, maudhui yaliyoonyesha dhima ya ndoa na watoto katika jamii, na umuhimu wa kudumisha maadili mema katika jamii, ingawa misingi ya maadili haya ilikuwa tofauti katika vipindi hivi viwili kama ilivyokwishajadiliwa. Licha ya kuendelea kwa baadhi ya maudhui, matokeo ya utafiti huu ni kwamba, kwa kiasi kikubwa, maudhui ya nyimbo za harusi za jamii ya Waembu yalibadilika kutoka kipindi cha kabla ya maingilio ya wakoloni yakilinganishwa na yale ya baada ya maingilio ya wakoloni kama ilivyobainika.

Mabadiliko haya ya maudhui kiwakati yanayodhihirika katika nyimbo za harusi za jamii ya Waembu yaweza kuelezwa kinadharia kwa kurejelea nadharia ya uhalisia ambayo imetumika kuongoza utafiti huu. Wataalamu wengi wa fasihi, akiwemo Qusby (1988), Larkin (1972:2), Lukacs (1972:6), Graig (1975:134-160), Wellek na Warren (1949:94-95)

wabainisha kwamba nadharia ya uhalisia huusawiri ulimwengu kama ulivyo wala siyo kama unavyofikiriwa kuwa. Kama nadharia ya uhakiki, uhalisia huzingatia namna ukweli unavyosawirika katika nyakati mbalimbali. Ukweli hubadilika kusawiri uhalisi katika jamii mbali mbali kutegemea historia ya wakati wake. Ukweli unaozungumziwa hapa hupatikana kupitia maudhui katika kazi ya fasihi.

Katika misingi hii ni bayana kwamba mabadiliko ya maudhui yaliyotokea kihistoria katika nyimbo za harusi za jamii ya Waembu yalitokana na mabadiliko yaliyoikumba jamii hii katika vipindi viwili tofauti. Nyimbo za kabla ya maingilio ya wakoloni zilikuwa na maudhui ya kitamaduni, kwani asasi za kitamaduni katika jamii hii zilikuwa imara na mwelekeo wa kitamaduni ulitawala shughuli zote za jamii ya Waembu. Baada ya maingilio ya wakoloni utamaduni wa Waembu uliathiriwa na dini ya Kikristo iliyoletwa na wakoloni, utangamano baina ya Waembu na wakoloni uliathiri maisha ya jumla ya Waembu, mwelekeo kuhusu ndoa ukiwapo. Haya yalichangia mabadiliko ya maudhui, kwani fasihi haitokei katika ombwe tupu, bali huchota maudhui yake katika jamii (Nandwa na Bukenya 1983). Yaliyoshuhudiwa hapa ni mabadiliko ya maudhui katika nyimbo za harusi za jamii ya Waembu kiwakati, huku nyimbo hizi zikionyesha uhalisi katika kipindi cha kabla ya maingilio ya wakoloni na cha baada ya maingilio ya wakoloni.

Maudhui yaliyoshamiri katika nyimbo za vipindi hivi viwili yalisawiri mwelekeo tofauti. Kabla ya maingilio ya wakoloni, maudhui katika nyimbo hizi yalichukua mwelekeo wa kitamaduni ambapo yalimsawiri mwanamke kama kitu hasi na kando, huku mwanamume akichukuliwa kama binadamu kielelezo. Baada ya maingilio ya wakoloni, harakati za wanaufeministi za ukombozi wa mwanamke zilishika kasi ambapo, kwa kiasi mtazamo kuhusu mwanamke katika jamii ulibadilika. Mtazamo huu pia ulichangia mabadiliko ya maudhui kiwakati katika nyimbo za harusi za watu wa jamii ya Waembu. Nadharia ya ufeministi wa Kiafrika iliyotumika, pamoja na ya uhalisia kuongoza utafiti huu yafafanua sababu za mabadiliko haya, haswa kwa kurejelea mihimili yake.

Maudhui yaliyoendelea kutoka kipindi kimoja hadi kingine yaweza kuelezwa kwa misingi ya nadharia ya umabadiliko kama mabaki ya hatua za kimaendeleo za hapo nyuma kama asemavyo Darwin mwasisi wa nadharia hii. Aidha, mabadiliko kiwakati hayatokei ghafla katika kazi yoyote ya fasihi. Pamoja na hayo, baadhi ya kazi za fasihi hupiku historia ya wakati wake, hivyo basi hazikumbwi na mabadiliko yoyote kihistoria. Hii ndiyo sababu baadhi ya maudhui hayakubadilika licha ya mabadiliko ya kihistoria katika jamii ya Waembu.

4.4 HITIMISHO

Sura hii imeshughulikia maudhui katika nyimbo za harusi za jamii ya Waembu za kabla ya maingilio ya wakoloni na baada ya maingilio hayo. Aidha, sura hii imeonyesha jinsi maudhui hayo yalivyobadilika na kuendelea kutoka kipindi kimoja hadi kingine. Mwisho, sura hii imeshughulikia maelezo ya matokeo ya utafiti kinadharia. Sura ya tano inayofuata inashughulikia muhtasari wa tasnifu, hitimisho na mapendekezo.

SURA YA TANO

5.0 UTANGULIZI

Sura hii inashughulikia muhtasari wa tasnifu kutoka sura ya kwanza kwenda ya nne. Pamoja na hayo, hitimisho jumuishi la mada pana ya tasnifu limetolewa. Mwisho, mapendekezo ya utafiti zaidi yameangaziwa pamoja na maoni ya mtafiti kuhusu matokeo ya utafiti.

5.1 MUHTASARI WA TASNIFU

Sura ya kwanza imeshughulikia mambo ya kimsingi kuhusiana na tasnifu. Mambo yaliyojadiliwa ni usuli wa mada ya utafiti, (chimbuko la Waembu, eneo la jamii ya Waembu kijiografia, jamii ya Waembu kabla ya maingilio ya wakoloni, swala la utafiti, maswali ya utafiti, nadharia tete, malengo ya utafiti, sababu za kuchagua mada ya utafiti, upeo wa utafiti, misingi ya nadharia, yaliyoandikwa kuhusu mada ya utafiti. Mbinu za utafiti, sampuli ya utafiti, mbinu za kukusanya data, mbinu za kuchanganua data na mbinu za uwasilishaji wa matokeo ya utafiti.

Sura ya pili imeshughulikia nyimbo za wakati wa sherehe ya harusi za jamii ya Waembu kabla ya maingilio ya wakoloni pamoja na maudhui anuwai katika nyimbo hizo, nyimbo zilizoimbwa baada ya harusi ya jamii ya Waembu kabla ya maingilio ya wakoloni pamoja na uchanganuzi wa

maudhui katika nyimbo hizo. Maudhui yaliyopatikana katika nyimbo hizo yalichanganuliwa kinadharia ambapo nadharia ya uhalisia na ile ya ufeministi wa Kiafrika zilikuwa msingi wa uchanganuzi.

Sura ya tatu imeshughulikia nyimbo za harusi za watu wa jamii ya Waembu zilizoimbwa kabla ya maingilio ya wakoloni, kuorodhesha maudhui hayo pamoja na kuchanganua maudhui katika kila wimbo. Mwisho, maudhui ya jumla katika nyimbo hizi yalibainishwa na kuorodheshwa pamoja na kuchanganuliwa kinadharia.

Sura ya nne imerejelea maudhui katika nyimbo za harusi za jamii ya Waembu kabla ya maingilio ya wakoloni, pamoja na maudhui bayana baada ya maingilio hayo, mabadiliko na maendeleo ya maudhui, matokeo ya utafiti na mwisho kueleza matokeo ya utafiti huo kinadharia.

5.2 HITIMISHO

Utafiti huu umeshughulikia mabadiliko ya maudhui kiwakati katika nyimbo za harusi za watu wa jamii ya Waembu za kabla na baada ya maingilio ya wakoloni katika jamii hii. Mabadiliko ya kimaisha ya jamii ya Waembu yalichangia katika mabadiliko ya jumla ya hali za jamii hii, huku mwelekeo wa watu kuhusu ndoa ukiwa mojawapo ya mabadiliko hayo. Mwelekeo tofauti kuhusu ndoa ulichangia pakubwa mabadiliko ya

maudhui katika nyimbo za harusi za jamii hii za kabla ya maingilio ya wakoloni na baada ya maingilio hayo. Ukweli ni kwamba maudhui hayo yalibadilika kusawiri uhalisia wa jamii katika kipindi husika kwa kuwa fasihi huchota maudhui yake katika jamii. Licha ya mabadiliko hayo, maudhui mengine yaliendelea kutoka kipindi cha kabla ya maingilio ya wakoloni hadi cha baada ya maingilio hayo kama mabaki ya kipindi kilichotangulia. Aidha, kutobadilika ghafla kwa mfumo wa maisha kuliyaafanya maudhui hayo kuendelea. Mabadiliko ya mwelekeo wa jamii hii kuhusu majukumu ya mwanamke na nafasi yake katika jamii yalichangia mabadiliko ya maudhui katika nyimbo za harusi za jamii ya Waembu, kwani maudhui haya yalimsawiri mwanamke kwa njia tofauti katika vipindi hivi viwili.

5.3 MAPENDEKEZO

Utafiti huu umeshughulikia mabadiliko ya maudhui kiwakati katika nyimbo za harusi za jamii ya Waembu za kabla ya maingilio ya wakoloni na baada ya maingilio haya. Nyimbo za harusi ni aina moja tu ya nyimbo katika jamii ya Waembu. Kuna nyimbo kama vile za tohara, za wakati wa kufanya kazi mbalimbali, wakati wa kutoa kafara, wakati wa shughuli za uganga wa kienyeji na zinginezo. Mapendekezo ni kwamba utafiti ufanywe katika nyimbo hizo.

Katika harakati za kukusanya data, ilibainika kwamba kuna maudhui anuwai yanayozagaa katika kategoria karibu zote za nyimbo zinazotekeleza majukumu mbalimbali miongoni mwa watu wa jamii ya Waembu. Utafiti zaidi wapaswa kufanywa kusudi kubainisha jinsi maudhui yanavyojengeka katika nyimbo zitekelezazo majukumu mbalimbali miongoni mwa watu wa jamii ya Waembu.

Aidha, ni muhimu kufanya utafiti wa kina kubaini kwa nini maudhui ya aina fulani yanaendelea hata baada ya mengine kubadilika kama ilivyobainika katika utafiti huu. Kuendelea huku kwaonyesha ukinzano wa fasihi na historia ya wakati wake, swala linalohitaji kufanyiwa utafiti, kwani hii ni kinyume na hali ya kawaida katika fasihi.

Utafiti huu umebainisha kwamba maudhui ya nyimbo, haswa za harusi katika jamii ya Waembu hubadilika na wakati kusadifu uhalisi wa jamii. Kutokana na haya, jamii yapaswa kutoa tahadhari kuhusiana na baadhi ya mabadiliko yaikumbayo jamii hii, kwani athari za kimagharibi katika jamii hii ambazo zimeanza kukita mizizi zitaleta uhalisi mpya utakaoyeyusha utamaduni wa harusi miongoni mwa watu wa jamii ya Waembu kupitia athari za maudhui katika nyimbo hizi, haswa tukizingatia kauli ya Njogu na Chimerah (1999) kwamba wimbo huwa na ushawishi mkubwa kupitia ujumbe wake. Wanajamii wapaswa kudhibiti

mabadiliko haya yasije yakasababisha uozo wa kijamii, haswa ikizingatiwa kwamba tamaduni nyingi za kimagharibi zinakinzana na utamaduni wa Kiafrika, haswa kimaadili.

MAREJELEO

Bukenya A, na Nandwa, J (1983). *African Oral Literature for Schools*. Nairobi. Longman Kenya.

Chesaina, C (1991). *Oral Literature of the Kalenjin*. Nairobi printing industries.

_____ (1999). "The Songs as a Medium of Expression of Gender Solidarity for Embu and Mbeere Women." Essay on Gender and Culture. Nairobi. K.O.L.A.

Chiuri, J. (1984). "Pop Music as a Form of Oral Literature" – a Survey of Joseph Kamaru (Tasnifu ya P.G.D.E – Chuo Kikuu cha Nairobi).

Embu District Development Plan (2007). "Effective Management for Sustainable Economic Growth and Poverty Reduction." Nairobi. Government Printers.

Finnegan, R (1970). *Oral Literature in Africa*. Nairobi. Oxford University Press.

George, M. (2005). "Mitazamo ya Utendakazi wa Nyiso Katika Jamii ya Watigania" (Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Kenyatta).

Creig, D. (1975). (ed) *Marxist on Literature*. London. Harmordsworth Peguine.

Kabira W.M. na Mutahi, K. (1988). *Gikuyu Oral Literature*. Nairobi. Heineman.

- King'ei na Kisovi, C. (2005). *Msingi wa Fasihi Simulizi*. Nairobi. Kenya Literature Bureau.
- King'ei (1992). Language, Culture and Communication, The Role of Swahili Taarab Songs in Kenya 1963 – 1990. U.M.I Dissertation Information Service of Bells Howen Information Company Michigan. U.S.A.
- Larkin, M. (1977). *Man and Society in the Nineteenth Century Realism*. London. Macmillan Press
- Lukacs, G. (1972). *Studies in European Realism*. A Sociological Survey of Writings of Balzac, Stredhal, Zola, Tolistoy, Gorki & Others. London. Marlin Press.
- Mbiti, J.S. (1975). *An Introduction to African Religion*. London. Heinemann.
- Mwaniki H.S.K (1969). *History of Embu and Mbeere*. Nairobi. African Literature Bureau.
- _____ (1974). *Embu Historical Texts*. Nairobi. East African Literature Bureau
- _____ (1986). *Categories and Substance of Embu Traditional Songs and Dances*. Nairobi. Kenya. Lit. Bureau
- Mwai, K.W (1997). “The Power of Song for Swahili Woman” Contesting Social Death. Essys on Gender and Culture. Nairobi. K.O.L.A

- Ndungo, C. (1985). "Wanawake na Mabadiliko ya Kihistoria Katika Fasihi ya Kiswahili." (Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu cha Kenyatta).
- Njogu K. na Chimera R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi, Nadharia na Mbinu*. Nairobi. Jomo Kenyatta Foundation.
- Nkonge, M (1988). "Literary Study of Songs of Joseph Kamaru. Theme and Style" (Tasnifu ya B.Ed Chuo cha Kenyatta).
- Okot, P'Bitek (1986). *Artist the Ruler*. Nairobi. Heineman Press.
- _____ (1973). *Africas Cultural Revolution*. Nairobi. Macmillan Books for Africa.
- Rimita, D (1988). *The Njuri Nceke of Meru*. Nairobi. Kolbe Press.
- Ruthven, K.K. (1984). *An Introduction to Feminist Literary Studies*. London. Cambridge University Press.
- Senkoro, F.G.M.K (1982). *Fasihi*. Dar-es.Salaam. Press and Publicity Centre.
- Swingerwood, A. (1991). *A Short History of Sociological Thought*. London. Macmillan Press.
- Yalwala, P. (1991). *Maudhui Katika Nyimbo za John Mwale* (Tasnifu ya M.A – Chuo Kikuu cha Nairobi).
- Wa Thiong'o, N. (1972). *Home Coming*. Heineman Educational Books.
- _____ (1986). *Decolonizing the Mind. The Policies of African Literature*. Nairobi. East Africa Literature Bureau.

Wamitila, K.W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi, Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi. Phoenix Publishers.

Wafula, R.M. (2004). "Sura Mbalimbali za Nadharia za Uhakiki Katika Usomaji na Uhakiki wa Fasihi." (Makala ya Semina Chuo Kikuu cha Kenyatta).

Wafula R.M. na Njogu K. (2007) *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi. Jomo Kenyatta Foundation.

Wellek, K.R. (1965). *A History of Modern Criticism 1750 – 1950 Vol III*. London. Cambridge University Press.

Werner, A. (1968). *Myths and Legends of the Bantu*. London. Fransisca and Co. Ltd.

KIAMBATISHO I

WALIOHOJIWA NA KUSHIRIKI KWA UIMBAJI

Runji Kubuta

Umri: 86

Tarafa: Nembure

Lokesheni: Gatari South

Kata: Nembure

Tarehe: 10/10/07

Kamwere Kubutu

Umri: 82

Tarafa: Manyatta

Lokesheni: Ngandori

Kata: Kigari

Tarehe: 13/10/07

Ileri Mathenge

Umri: 72

Tarafa: Kyeni

Lokesheni: Kagaari

Kata: Mufu

Tarehe: 15/10/07

Kiringa Rurii

Umri: 75

Tarafa: Kyeni

Lokesheni: Kathanjuri

Kata: Kathari

15/10/07

Mbaka Njue

Umri: 78

Tarafa: Runyenjes

Lokesheni: Kagaari

Kata: Kigaa

Tarehe: 15/10/07

Ciumwari Kagereki

Umri: 79

Tarafa: Runyenjes

Lokesheni: Kagaari

Kata: Ngeniari

Tarehe: 17/10/07

Nguri

Umri: 76

Tarafa: Central

Lokesheni: Municipality

Kata: Iveche

Tarehe: 19/10/07

Matenguri Mwita Njau

Umri: 90

Tarafa: Central

Lokesheni: Municipality

Kata: Kangaru

Tarehe: 19/10/07

Mugo Nginyirwa

Umri: 76

Tarafa: Nembure

Lokesheni: Gatari South

Kata: Nembure

Tarehe: 20/10/07

George Sogoria

Umri: 96

Tarafa: Manyatta

Lokesheni: Ngandori

Kata: Kigari

Tarehe: 13/10/07

Kwaya ya Kanisa Karingari

Tarehe: 21/10/07

Kikundi cha Akina Mama cha *Murugi*

Tarehe: 22/10/07

Washiriki katika harusi ya Sally Munyi na Carol Murugi


Tarehe: 24/10/07

Washiriki katika harusi ya Justa Muthoni na Kinyua Nthambiri

Tarehe: 24/10/07

KIAMBATISHO II

Ramani ya Eneo la Utafiti – Wilaya ya Embu




Source: Embu District Profile 2007

KIAMBATISHO III



Baadhi ya walioshiriki katika uimbaji wakiimba

Waimbaji wakijitambua kumbwa



Shughuli ya uimbaji ikiendelea

Mtaji akishirikiana na waimbaji

KIAMBATISHO IV



Waimbaji wakijitayarisha kuimba



Mtafiti akishirikiana na waimbaji

KIAMBATISHO V



Uimbaji ukiendelea



Muimbaji akijitayarisha kuimba